# Nipashe

Jumatatu Januari 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580132

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## NSSF yakabidhi majengo 32 wanafunzi vyuo vikuu 4,300

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wengi waachwa

• **Ni** leo simu zao zitakapozimwa kwa kukosa vitambulisho vya Taifa, vilio vyatawala kila kona kwamba...*Endelea ukurasa 2*



Wananchi wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga wakiwa wame-panga foleni katika ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) mjini Kahama jana, kutafuta vitambulisho. **PICHA: NDALIKE SONDA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Mgombea mwanamke Chadema atajwa kumvaa JPM urais

UKURASA 4

## Ofisa elimu ashtakiwa mamilioni fedha za madawati

UKURASA 2


**MICHEZO** ZIDANE: APONGEZA VAR KUKATAA BAO LA DE JONG UK.29

MAONI, KATUNI UK.6

## ‘Kuchimba dawa’ ovyo faini 200,000/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepiga marufuku mabasi ya abiria kuruhusu abiria kuchimba dawa (kujisaidia) kwenye maeneo yasiyo rasmi, na kwamba endapo wakibainika watapigwa faini ya Sh. 200,000 au kifungo cha miezi sita jela.

Sambamba na hilo, imeagiza mabasi hayo kupuliziwa dawa za kuua wadudu ikiwamo kunguni ndani ya siku saba kwa kuwa wamekuwa wakiwadhuru abiria.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Afya wa Jiji la Dodoma, Abdallah Mahiya, katika ukaguzi wa mabasi yaendayo mikoani pamoja na usafi wa maeneo ya mama ntilie kwenye kituo cha mabasi cha Nanenane.

Alisema kumekuwa na tabia ya mabasi kusimama ovyo na abiria wakijisaidia kwenye maeneo yasiyo rasmi hali inayochangia uchafu wa mazingira.

“Kwa mujibu wa sheria ni marufuku kwa mtu yeyote abiria au mmiliki wa gari kujisaidia sehemu isiyo rasmi na faini yake ni Sh. 200,000 au kifungu cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja,” alisema.

Mahiya aliwataka wananchi kuhakikisha hakuna basi linalosimama maeneo ambayo hakuna vyoo kwa kuwa ni jambo la hatari kwa wakazi wa maeneo hayo kwa watu kujisaidia ovyo.

“Basi linasimama maeneo ya watu au kwenye shule watu wanajisaidia halafu watoto wanaosoma pale wakiwa wanafanya usafi wanashika vinyesi vyao jambo ambalo ni hatari kwa afya,” alisema.

Aidha, alisema katika ukaguzi huo wamebaini mabasi kuwa na wadudu dhurifu kama vile kunguni, mende na kuwataka ifikapo Januari 24, mwaka huu yawe yamepulizwa dawa za kuua wadudu hao. “Tumefanya ukaguzi kwa mabasi zaidi ya 20 hadi sasa tumebaini mengi hayapuliziwi dawa za kuua wadudu, vizima moto vingi havitumiki kuna nyingine hazina vizima moto baadhi vimekaa kama maonyesho, pia visanduku vya kuhifadhia dawa za huduma ya kwanza hakuna vingine vina upungufu havina dawa,” alisema.

Aliagiza kila basi kuhakikisha lina kisanduku cha huduma ya kwanza na dawa zinazotakiwa.

“Si kuwa tupu waweke wembe maalum za upasuaji si kuwa na wembe wa kawaida, vitunza taka viwapo na vitumike si kuwekwa kama urembo na madereva waache tabia ya kutupa taka ovyo njiani,” alisema.

Kuhusu usafi maeneo ya vyakula, alieleza kuwa wafanyabiashara wengi wanazijua sheria, lakini wanazipuuza kwa kutovaa sare wakati wa kuhudumia wateja na kutozingatia kanuni za usafi.

# Wengi waachwa, simu kuzimwa leo

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI leo ndiyo siku ya mwisho kwa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole, idadi kubwa ya Watanzania wameachwa baada ya kushindwa kupata namba za Vitambulisho vya Taifa kutekeleza agizo hilo.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Semu Mwakyanjala, alisema hadi Januari 15, watu milioni 27, 287,009 sawa na asilimia 56 walishasajiliwa.

Alisema wananchi ambao hawajasajiliwa ni milioni 21,243, 876 sawa na asilimia 44, huku idadi ya wamiliki wa laini za simu ikiwa ni milioni 48,717,967.

Desemba 27, mwaka jana Rais John Magufuli akiwa mapumzikoni nyumbani kwake Chato mkoa wa Geita, alitangaza kuongeza siku 20 kwa watu wote watakaoshindwa kusajili laini zao ifikapo Desemba 31, mwaka jana, kuanzia Januari leo.

Hadi kufika jana jioni Nipashe ilikuta msururu wa wananchi wakiingia katika ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) ili kupata namba zitakazowawezesha kusajili laini zao.

Idadi kubwa ya wananchi hao walionekana wakiwalalamikia maofisa wa Nida kwa kushindwa kuwahudumia, huku wengine wakimwomba Rais Magufuli kuongeza muda wa uandikishaji wa kupata vitambulisho.

**MOROGORO**

Nipashe lilipita katika badhi ya mitaa na kukuta msongamano mkubwa katika vituo, huku baadhi kutokuwa na mashine za kutosha kuwahudumia wananchi.

Baadhi ya wananchi hao na mawakala wa uandikishaji, wamelalamikia kampuni moja ya simu kuwa na mlolongo mrefu wa usajili.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa wananchi, Jackson Mchanjali, alisema licha ya foleni ndefu katika vituo vya uandikishaji, hana uhakika kama atafanikisha uandikishaji kutokana na msongamano huo pamoja na mashine zilizopo kufanya kazi kwa taratibu.

“Wakiingia watu watano hadi watoke wanatumia zaidi ya saa moja, mashine hapa kwenye kituo ni moja tu, sasa sijui kama tutafanikisha usajili,” alisema Mchanjali.

Mwananchi mwingine, Mbegu Mohamed, alimwomba Rais Magufuli kuongeza muda badala ya kuzima simu kwani itawaathiri watumiaji wengi wa simu za mkononi kwa vile wengi wao hawajasajili kutokana na changamoto zinazoendelea.

Akizungumzia kero hiyo, Ofisa Msajili wa Nida Mkoa wa Morogoro, James Malimo, alisema changamoto kubwa ya foleni imesababishwa na wingi wa watu waliojitokeza siku za mwishoni huku wengine wakiwa ni wateja wapya.

**SHINYANGA**

Nipashe lilitembelea baadhi ya mitaa wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga na kukuta idadi kubwa ya wananchi wakiwa wanalalamika kutokupata namba za kitambulisho cha Nida.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi hao walisema kuwa kazi ya utoaji namba za kitambulisho haliwezi kufanikiwa kutokana na changamoto mbalimbali kutoka Nida.

INAENDELEA UK.8



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (aliyevaa kofia nyeusi), akikagua miundombinu ya reli ya Moshi - Arusha eneo la Rundugai ambayo amedai kuna watu wameunda genge la uhalifu kuihujumu. **PICHA: GODFREY MUSH**

# Ofisa elimu ashtakiwa wizi fedha za madawati

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) Mkoa wa Dodoma, imemfikisha mahakamani Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Stephano Ndabazi (44), kwa tuhuma za kujipatia Sh. milioni 24.3 kwa njia ya udanganyifu.

Imeelezwa kuwa fedha hizo zilichangwa kwa ajili ya kununua madawati.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema Ndabazi alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma na alitenda kosa hilo akiwa Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mpwayungu Wilaya ya Chamwino kinyume cha kifungu 273(b) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu sura ya 16 marejeo ya 2002.

Kibwengo alisema ofisa huyo anatuhumiwa kuiba kiasi cha Sh. 24,334,920, Aprili, mwaka 2016, wakati akiwa shuleni hapo.

“Katika uchunguzi wa Takukuru umeonyesha akiwa mjumbe wa kamati ya madawati, Ndabazi alijipatia kwa njia ya udanganyifu fedha hizo zilizochangwa na wananchi na wahisani kwa ajili ya kununua madawati ya shule za Wilaya ya Chamwino zikiwa ni sehemu ya michango ya zaidi ya Sh. milioni 85,” alisema.

Alieleza kuwa kesi hiyo namba 9 ya mwaka 2020 ilisomwa mbele ya Hakimu Mkazi Pascal Mayumba na mshtakiwa huyo ameachiwa kwa dhamana hadi Februari 21, mwaka huu.

**MWINGINE ASIMAMISHWA**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita limemsimamisha kazi Ofisa Elimu Msingi wa halmashauri hiyo, Said Matiku, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma anazotuhumiwa ikiwamo

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA

# Wakurugenzi wapewa mtihani fedha kielektroniki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mhandisi Joseph Nyamhanga, amewataka wakurugenzi wa halmashauri, kuongeza usimamizi katika fedha zinazokusanywa kupitia mfumo wa kielektroniki ili kuondoa kero zinazowakabili wananchi.

Nyamhanga alitoa maelekezo hayo alipokuwa akifungua semina na mkutano mkuu wa wanachama wa Jumuiya ya Ushirikiano wa wataalamu wa Tanzania na Osaka Japan (TOA) unaofanyika jijini Dodoma.

Alisema wakurugenzi hao wanatakiwa kuongeza usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kupitia mifumo ya kidijitali ili kusaidia kuongeza mapato ya ndani.

"Msimamie hizi fedha ili zileta tija katika kuboresha maeneo mbalimbali ya nchi ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na changamoto nyingi za huduma kama afya, maji pamoja na elimu," alisema Nyamhanga.

Aidha, aliwataka wakurugenzi hao kuhakikisha wanasimamia kwa karibu fedha zinazotolewa na serikali katika kutekeleza miradi mbalimbali ili ikamilike kwa wakati.

"Moja ya changamoto kubwa ni miradi kutokamilika kwa wakati hali ambayo inachangia hata Wizara ya Fedha kusimamisha baadhi ya miradi ambayo inachelewa kukamilika kutokana na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji," alisema.

Alisema katika eneo hilo wakurugenzi wengi wameshindwa kutimiza wajibu wao, hali ambayo imesababisha wengi wao kusimamishwa, kufikishwa kwenye vyombo vya sheria na wengine kuondolewa nyadhifa zao.

Pia Nyamhanga alisema bado baadhi ya wakurugenzi wanashindwa kufanya matumizi ya mfumo wa 'Force Account'.

Alisema wakurugenzi wanatakiwa kutumia mwongozo mpya uliotolewa na Tamisemi, unaoelekeza matumizi sahihi ya utaratibu huo.

"Hivi sasa katika utaratibu wa force account kumekuwapo na changamoto ya vifaa kununuliwa kwa bei ya juu, lakini upendeleo kwa hawa mafundi tunaowatumia," alisema Mhandisi Nyamhanga.

Vilevile aliwataka wakurugenzi wote kuhakikisha kuwa wanakamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kuondoa msongamano ulipo katika shule mbalimbali.

"Tuhakikishe kuwa tunakamilisha vyumba vya madarasa katika muda uliopangwa ili kuondoa changamoto ya msongamao ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2020," alisema.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wanachama wa TOA, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Rehema Madenge, alisema watahakikisha wanaitumia jumuiya hiyo kupeleka maendeleo kwa wananchi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (wa pili kulia) pamoja na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Jocye Ndalichako (wa kwanza kulia), wakiangalia moja kati ya tangi la maji ikiwa ni moja kati ya miundombinu katika maeneo hayo ya makazi ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya NSSF, Balozi Ali Idi Siwa (wa kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio (wa pili kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# NSSF yakabidhi majengo 32 wanafunzi vyuo vikuu 4,300

**Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limekabidhi majengo 32 ya ghorofa yaliyopo eneo la Mtoni Kijichi jijini Dar es Salaam kwa ajili ya vyuo vikuu sita ambayo yatakaliwa na wanafunzi zaidi ya 4,314.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, aliyasema hayo juzi wakati wa makabidhiano ya majengo hayo kwa ajili ya kutumika na wanafunzi wa elimu ya juu kwa baadhi ya vyuo jijini Dar es Salaam, kama mabweni yao mapya.

Makabidhiano hayo yamekuja siku chache tangu kuingia mkataba baina ya vyuo hivyo na NSSF kwa ajili ya majengo hayo kutumiwa na wanafunzi kama hosteli.

Aidha, waliwashukuru wakuu wa vyuo vya elimu ya juu kwa utayari wao katika utekelezaji wa mradi tangu walipoanza katika hatua ya mazungumzo ya awali na baadaye kusaini makubaliano ya awali.

Alisema wanazo nyumba ambazo zinafaa kwa ajili ya walimu na watumishi wengine, na kuwataka wakuu hao wa vyuo kuchangamkia fursa ya uwapo wa nyumba hizo ili kupata makazi bora.

Kaimu Ofisa Tarafa Mbagala, Theodota Marata, alisema katika mradi huo Temeke ni wanufaika wakubwa, kwa kuwa utasaidia vijana wengi hasa wa vyuo vikuu ambao walipata hadha kubwa ya hosteli. "Makabidhiano haya yataenda kuokoa jahazi hili na kuwasaidia wanafunzi wetu kwenda kupata makazi mazuri," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya NSSF, Balozi Ali Siwa, alisema mradi wa Mtoni Kijichi utakuwa na mabweni una ghorofa 64 zenye jumla ya nyumba 720.

Alisema ghorofa 32 zenye nyumba 356 zinazokadiriwa kuchukuwa wanafunzi 4317, zimekabidhiwa kwa vyuo vitano.

Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Elimu (DUCE) kitachukua ghorofa tano kwa ajili ya wanafunzi 696, IFM ghorofa sita wanafunzi 815, DIT ghorofa moja linaloingia wanafunzi 144, Taasisi ya Uhasibu (TIA) ghorofa 10 za wanafunzi 1,165, Chuo cha Diplomasia kitachukua ghorofa moja la wanafunzi 96 na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ghorofa tisa za wanafunzi 1,398.

Hivi karibuni, akikabidhi mabweni hayo kwa wanafunzi, Waziri Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema serikali itahakikisha tatizo la makazi ya wanafunzi linapatiwa ufumbuzi na kuwa historia nchini.

"Kupitia mradi huu NSSF imekuwa jibu sahihi la kuondoa tatizo la makazi na malazi kwa wanafunzi," alisema.

Aidha, alionya nyumba hizo zisigeuzwe mradi wa vyuo vikuu, na badala yake gharama za upangishaji zitumiwe na wanafunzi wa hali zote.

Kwa mujibu wa Mhagama, serikali haitawafumbia macho ambao watakwamisha watoto wa hali zote kuishi katika nyumba hizo.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alishukuru NSSF kwa kutoa majengo hayo ambayo yatatatua kero zinazowakabili wanafunzi wa elimu ya juu jijini humo.

Alisema tatizo la makazi kwa vijana wanaosoma elimu ya juu ni kubwa na kwamba asilimia kubwa wanaishi nje ya vyuo vyao, hivyo kushindwa kuhudhuria vipindi na kuwa na utulivu katika masomo.

# Muhimbili yatumia bil. 1.9/- kusomesha wataalamu nje

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imetumia Sh. bilioni 1.9 za kupeleka wataalamu wake nje ya nchi kujifunza mbinu za kutibu magonjwa yalisiyotibika nchini kwa lengo la kupunguza rufani za nje ya nchi.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu wa Muhimbili, Dk. Hedwiga Swai, wakati akizungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la ziara hiyo ni kutembea taasisi hizo na kuangalia mafanikio ya miaka minne ya serikali ya awamu ya tano katika sekta ya afya.

Alisema fedha hizo zilizotumika zimesharudi kutokana na kiasi cha fedha kilichookolewa kwa wagonjwa waliokuwa waende kutibiwa nje ya nchini katika kipindi cha miaka hiyo minne.

Alisema rufani walizopunguza ni za wagonjwa wa kupandikizwa vifaa vya kusikia huduma iliyoanza mwaka 2017 na kabla ya hapo walikuwa wakipata huduma nje ya nchi kwa Sh. milioni 100, lakini MNH wanatoa huduma hiyo kwa Sh. milioni 35.

"Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2003 hadi 2016 serikali ilipeleka wagonjwa 50 nchini India, lakini kwa miaka miwili MNH imewafanyia upandikizaji wagonjwa 34 waliogharimu Sh. bilioni 1.3 na kama wangeenda nje ya nchi wangetumia Sh. bilioni 3.4 hivyo tumeokoa Sh. bilioni 2.2," alisema Dk. Swai.

Alisema pia huduma nyingine inayotolewa MNH ni matibabu ya uvimbe wa taya kwa kutumia mionzi na tayari wagonjwa 302 wamepatiwa huduma tangu mwaka 2017 kwa gharama ya Sh. milioni nane kwa mgonjwa mmoja na kama angeenda nje ya nchi ingemgharimu Sh. milioni 100.

Dk. Swai alisema pia huduma ya kurekebisha mifupa ya uso na taya ambayo hadi sasa wagonjwa 120 wamenufaika kwa gharama ya Sh. milioni 3.5 kwa mgonjwa mmoja na kama angeenda nje ya nchi ingemgharimu Sh. milioni 70.

Alisema pia wanaendelea kuboresha huduma kwa kununua vifaa vya kisasa vya kutoa matibabu ya kibingwa nchini, ikiwamo mashine ya kisasa ya Ultrasound kwa ajili ya kuchukulia kipimo cha tezi dume mbadala wa kutumia vidole iliyonunuliwa kwa Sh. milioni 70.

Alisema pia wapo katika maandalizi ya kupandikiza mimba na ukarabati wa jengo utaanza hivi karibu kwa gharama ya Sh. milioni 383, na kwamba wataalamu wameshapelekwa nchini India kujifunza namna ya kuendesha huduma hiyo.

MAHOJIANO MAALUM

# Mgombea mwanamke Chadema atajwa kumvaa JPM urais 2020

Na Enock Charles

IKIWA imebaki takriban miezi minane kuanza kwa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, ameingia kwenye orodha ya wanaotajwa kuwa na nafasi ya kupeperusha bendera ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika kuwania kiti cha urais mwaka huu.

Kwa muda mrefu sasa, aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu (Chadema), amekuwa akitajwa kuwa na nafasi kubwa ya kuwania nafasi hiyo mwaka huu, hasa ikizingitiwa, amekuwa mkosoaji mkubwa wa serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, ambaye ana nafasi kubwa ya kuteuliwa na chama chake (CCM) kuwania tena nafasi hiyo.

Lissu, ambaye amekuwa akiishi ughaibuni kwa takriban miaka miwili sasa, amekaririwa mara kwa mara akisisitiza yuko tayari kuwania nafasi hiyo endapo chama chake kitaona anafaa kuwa mgombea wa nafasi hiyo kubwa zaidi ya uongozi nchini.

Wakati wadau wa siasa za Tanzania na Afrika Mashariki wakisubiri kuona na kusikia jina la mgombea urais wa Chadema mwaka huu, jina la Mbunge wa Kawe, nalo limepenya kwenye orodha.


Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (Bavicha), Moza Ally, alimtaja Mdee kuwa na sifa na nafasi ya kuteuliwa kuwania nafasi hiyo kupitia chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Alisema kwa mtazamo wake, anaona mbunge huyo ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha) na Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, anafaa kuwa mgombea wa kiti cha urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Hata hivyo, Nipashe ilipomtafuta Mdee kuzungumzia suala hilo, alisema kwa sasa hana mpango wa kuwania nafasi hiyo licha ya kwamba anazo sifa zote zinazohitajika kikatiba kuwania nafasi hiyo, ikiwa ni pamoja na kuwa na umri unaovuka miaka 40, akiwa na umri wa miaka 41 kwa sasa.

"Nipo nje ya nchi Enock, lakini nafasi ya urais ni nafasi ambayo mtu yeyote mwenye sifa na aliyetimiza miaka 41 anaweza akagombea, lakini kwa sasa sina 'plan' (mpango) hiyo na siwezi kusemea kwa baadaye kwa sababu siwezi kujua kwamba nitakuwa hai au nimekufa," Mdee alisema.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na Makamu Mwenyekiti wa Bavicha, Moza, aliyeibua suala la Mdee kuwania urais mwaka huu:



Makamu Mwenyekiti wa Bavicha, Moza Ally.

**SWALI: Katika chama chenu kuna wanasiasa wengi na wazuri. Je, ni yupi kati yao, unafikiri anafaa kupeperusha bendera ya Chadema kuwania kiti cha urais mwaka huu?**

**MOZA:** Kiukweli kabisa wapo wengi, lakini mimi ninawafikiria wawili

Halima Mdee na Tundu Lissu. Hawa naona wanafaa zaidi kwa wakati huu.

**SWALI: Ni kwanini uliamua kugombea nafasi hii?**

**MOZA:** Ni kwa sababu niliona nahitaji kukisaidia chama kwenye upande wa vijana. Niliona nina uwezo huo kuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Taifa kwa ajili ya kuwaandaa na kuwatia moyo vijana, hasa wa kike kwamba inawezekana kushika nafasi kama hii na kuitendea haki.

Upungufu sijaona isipokuwa kwa muda mrefu hapajatokea kiongozi mwanamke katika kushika nafasi kama hii. Sababu inajulikana kwamba bado wako nyuma kwenye masuala ya siasa kutokana na hofu.

Mimi sasa nipo kwenye chama, nikaona tunawahitaji hawa mabinti waingie katika siasa, wanahitaji binti mwenzao ambaye anaweza kuwa kiungo. Kwa hiyo, nikajitathmini, nikaona 'I can' (ninaweza), ndiyo maana nikaomba nafasi hii.

**SWALI: Kwa hali ya kisiasa ilivyo nchini kwa sasa, Chadema itarudi na nguvu ileile baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu?**

**MOZA:** Kiukweli kabisa hakuna wakati ambao Chadema imejitengeneza kama huu. Ina mizizi mirefu sana chini. Unajua mikutano ya kisiasa ilipozuiwa, kuna kitu kikaanzishwa na Mwenyekiti wetu Taifa (Freeman Mabowe), kinaitwa Chadema ni Msingi.

Kwa kweli kile kitu ni kizuri sana sana na pongezi kwa Mwenyekiti wetu kwa sababu alifikiria kwamba mikutano ya kisiasa sasa tumenyimwa na ili tuwafikie watu, wakatoka viongozi wa kitaifa, wakaenda kwenye 'grassroots' chini kabisa, tumejitahidi kumfikia kila Mtanzania na kiukweli huko tunakoelekea CCM wajipange sana.

**SWALI: Unafikiri nini kifanyike ili kuing'oa CCM madarakani?**

**MOZA:** Kitu kikubwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inatakiwa kufahamu ni kwamba Watanzania si waoga. Lazima wafahamu kwamba bila tume huru ya uchaguzi, basi wataweza kuongoza hii nchi milele.

'This time' (wakati huu) hatuwezi kwenda tena kama ilivyokuwa hapo nyuma, huu ni uchaguzi mkuu unaohitaji kila Mtanzania kufanya uamuzi wa miaka mitano ili kujua mustakabali mzima wa nchi yetu.

**SWALI: Kipaumbele cha Chadema sasa kinaonekana wazi ni kudai tume huru ya uchaguzi. Je, isipopatikana hamtashiriki uchaguzi?**

**MOZA:** Kama tume huru haitapatikana, iliyopo italazimishwa iwe huru kwa namna tofauti sana watu wanatakiwa wasubiri waone. Italazimishwa iwe huru, watawala wajiandae tu, waache Watanzania waamue kiongozi wanayemhitaji, wachague wenyewe wanataka waongozwe na nani.

Sisi tuna 'slogan' yetu inaitwa 'People's Power', yaani nguvu ya umma na sasa hivi tumeijenga kwelikweli, tulivyonyimwa mikutano ya hadhara na kama tuliweza asilimia mia moja kusimamisha viongozi wa serikali za mitaa mpaka wakawa wanawaambia hawajui kusoma na kuandika na wengine wao waliwahi kuwa viongozi, sijui waliongoza vipi kama hawajui kusoma na kuandika.

**SWALI: Ni jambo gani zuri unaloona limefanywa na serikali ya sasa?**

**MOZA:** Kiukweli, kikubwa ninachokiona sana sana ni maumivu makubwa kwa Watanzania. Angalia watu wengi, hasa vijana wamekosa ajira, vijana walioko vyuoni wanakosa mikopo kwa wakati na wakidai mikopo yao wanafunguliwa mashtaka ya hapa na pale na kufukuza chuoni.

**SWALI: Ukipata nafasi ya kuzungumza na Rais John Magufuli kwa dakika moja, utamweleza jambo gani muhimu kwa nchi?**

**MOZA:** Kitu nitakachomwambia Rais ni kimoja tu, Watanzania wanahitaji tume huru ya uchaguzi. Hili jambo la msingi kwangu kwa Rais.

**SWALI: Ni mipango gani uliyonayo katika siasa kwa siku zijazo?**

**MOZA:** Mungu akinijalia, akiniweka hai, nina mipango ya kupigania hii nchi, nina 'spirit' kubwa sana na imani yangu ni ya kuhamisha milima, Mungu akipenda nataka kuwa rais wa hii nchi, nitatia nia chama kikinipa nafasi muda ukifika.

**SWALI: Watanzania wangependa kufahamu historia yako. Tueleze kwa kifupi.**

**MOZA:** Mimi ni binti wa tatu kwenye familia ya mabinti wanne. Elimu yangu ni ya Chuo Kikuu (Shahada ya Usimamizi wa Biashara) na pia nina Diploma ya Information Technology, shule ya msingi nilisoma Monduli, sijaolewa na sina mtoto.

**SWALI: Je, unawezaje kugawa muda wako kati ya mambo ya siasa na shughuli zako binafsi?**

**MOZA:** Nikwambie katika maisha kila kitu ni siasa, siasa ni uchumi na kama ni uchumi lazima uipe muda mzuri tu na siasa haikubani, yaani watu wasidanganye watu kuwa siasa inaweza ikakubana ukashindwa kutafuta ugali, ukashindwa kwenda kwenye majukumu ya kufanya biashara zako muda.

Lazima kuna muda utapata wa kwenda kutafuta ugali na muda wa kufanya siasa. Muda wangu kwenda kuwatumikia vijana walioniamini na muda wa kwenda kutafuta ugali wangu upo.

**SWALI: Kabla ya kuwa mwanachama wa Chadema, uliwahi kuwa mwanachama wa chama kipi kingine?**

**MOZA:** Nimekuwa mwanachama wa Chadema tangu mwaka 2012, sijawahi kuwa mwanachama wa chama kingine chochote na wala sitarajii, Mungu anisaidie sana.

**SWALI: Ni vikwazo vipi vinavyowakabili wanawake katika siasa?**

**MOZA:** Vikwazo ni vya kawaida. Kwa mfano, unaweza ukawa unajulikana sana, watu wanakufahamu sana, lazima wanatokea wanaume wanaopenda kusumbua tu, lakini si kwamba wana nia ya kweli ya kuwa na wewe, lakini wanasumbua tu.

Vikwazo hivyo hivyo havinibabaishi kwa sababu mimi ninajua ninachokifanya, nina 'focus' kwenye maisha yangu, ninatengeneza maisha yangu na kuwa kwenye siasa, kikubwa ninachojua siasa 'is life' (siasa ni maisha), tena 'is a good life' (ni maisha mazuri), yaani nafurahia kuwa mwanasiasa.

**SWALI: Una ushauri upi kwa vijana wanaofikiri kuwa wanasiasa kama wewe?**

**MOZA:** Kikubwa ni kuwa na moyo wa utayari na kwa sasa tangu awamu ya tano iingie madarakani, siasa kila mtu anione ni kitu kigumu, yaani sikufichi, lazima kila mtu uwe una utayari.

Kama tumeona kuna viongozi wanapoteza mali zao, wanapoteza kazi zao, kama mimi kwa mfano ni mwajiriwa sehemu fulani, anaweza mwajiri wangu asiridhike na mimi kufanya siasa, lakini kisheria unaruhusiwa ili mradi tu utenge muda wa kazi zako ni upi na wa kufanya siasa ni upi, kisheria inaruhusiwa.

**SWALI: Bavicha ya sasa imejipangaje kukabiliana na usaliti ikizingatiwa kuwa kiongozi mkubwa wa umoja huu katika awamu iliyopita, alikiacha chama na kuhamia kwingine?**

**MOZA:** Kila mtu ana haki ya kuchagua upande anaouhitaji kisheria kabisa, ipo wazi kwamba mtu anajua kwamba ninaweza nikawa Chadema au chama kingine, ni haki yake ya kikatiba.

Lakini, kama amechaguliwa na watu, mfano mbunge au diwani, watu wamepanga kabisa mstari kuanzia asubuhi mpaka jioni na wakayalinda matokeo, hata kama ni haki yako ya kikatiba, kwamba uchague, lakini unawaumiza vipi wale watu waliohakikisha hadi kura zako zikatosha?

**SWALI: Ni mikakati ipi ambayo Bavicha inayo katika kudai tume huru ya uchaguzi?**

**MOZA:** Mikakati tayari ipo, tumeshaanza nayo taratibu, muda ukifika tutaitoa, tutawaeleza. Kwa sasa hivi siwezi nikawaambia, lakini tayari mikakati ya kudai tume huru ya uchaguzi tumeshaanza nayo.

Nawaomba tu Watanzania wawe na imani na Bavicha na uongozi wetu wa sasa, ni watu wanaofuatilia jambo si wa kukurupuka.

# Majaliwa atoa neno mradi ukarabati hoteli

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua mradi wa ukarabati wa hoteli ya Mkoani ambapo amesema lengo la maboresho hayo ni kuimarisha shughuli za utalii na kupunguza tatizo la ajira.

Amesema ili kuhakikisha lengo la serikali linafikiwa amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Khamis Mussa Omar, ahakikishe mradi huo unakamilika kwa wakati ili kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

Ameyasema hayo jana baada ya kukagua mradi huo uliopo katika Wilaya ya Mkoani mkoa wa Kusini Pemba. Mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni nne unatekeleza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Waziri Mkuu alisema mradi wa ukarabati wa hoteli ya Mkoani ni muhimu katika kuimarisha sekta ya utalii na huduma za malazi hususani kwa wageni wanaotembelea kisiwa hicho cha Pemba sambamba na kutengeneza ajira kwa wanawake na vijana.

"Ukarabati huu unatarajia kutoa mchango mkubwa katika kukuza sekta ya ajira, teknolojia, kuongeza mapato ya serikali na kuimarisha ustawi wa wananchi wetu. Endeleeni kuiamini serikali yenu."

Akisoma taarifa ya ukarabati wa mradi huo, Meneja Uwekezaji wa ZSSF, Abdulaziz Ibrahim Idd, alisema ukarabati huo ulianza Julai 2019 na unatarajiwa kukamilika Machi 2020. Amesema ukarabati wa jengo hilo ambalo awali lilikuwa la ghorofa moja umehusisha pia kuongeza ghorofa mbili na kufikia tatu, hali ambayo italifanya jengo hilo kuwa na vyumba 16 vya kulala kutoka vinane vya awali vikiwamo viwili kwa ajili ya watu mashuhuri. Meneja huyo amesema kuwa mbali na kuongezeka kwa vyumba pia umejengwa ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 100, mgahawa wa kisasa pamoja na sehemu ya kufulia nguo kwa ajili ya wageni na watu wote watakaohitaji huduma hiyo.

"Kwa sasa ujenzi huu umefikia asilimia 80 na unatarajia kukamilika mwezi Machi mwaka huu. Mradi huu utakapokamilika utakuwa ni moja ya chanzo cha ajira za kudumu 50, hivyo kuinua uchumi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla."

Hoteli hiyo inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifunguliwa Septemba 1974 na iliendeshwa na serikali yenyewe kwa lengo la kutoa huduma kwa wageni na hata wenyeji waliofika Pemba.

Lakini kutokana na uchakavu wake, serikali ikaamua kusitisha huduma zake na kuifunga ili kutafuta mwekezaji ambaye ataiendeleza. Hoteli hiyo imekuwa haitumiki kwa kipindi cha takribani miaka 12.

Hata hivyo, Baraza la Mapinduzi chini ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein likaamua kuikabidhi ZSSF hoteli hiyo kwa lengo la kuifufua na kuiendeleza.

# M'nyamala yajigamba kumaliza kero wazazi

Na Mary Geofrey

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyama, imeeleza namna ilivyofanikiwa kuondoa kero walizokuwa wakizipata wajawazito na wazazi waliokuwa wakijifungua.

Aidha, imefanikiwa kutumia kondo la nyuma la uzazi la wanawake wanaojifungua, kuzalisha gesi inayotumika kuchemsha maji ya kuwahudumia.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mwananyamala, Mussa Wambura, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kundi hilo lipo kwenye ziara ya kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya' yenye lengo la kuelezea mafanikio ya miaka minne ya serikali ya awamu ya tano katika sekta hiyo.

Alisema kutokana na kuwapo kwa huduma hiyo, kumemaliza changamoto ya wanawake kubebeshwa ndoo za maji ya moto kutoka nyumbani na kondo walilokuwa wakifungashiwa kurudi nalo nyumbani kuyatupa.

Alisema huduma hiyo ilianza mwaka 2018 baada ya Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kununua na kufunga mashine hiyo ambayo haipatikani hospitali yoyote nchini zaidi ya Mwananyamala.

Alisema kwa siku wanawake 40 hadi 60 wanajifungua katika hospitali hiyo sawa na wanawake 900 hadi 1,200 kwa mwezi, hivyo hutumia kondo kuzalisha kiasi kikubwa cha gesi. "Mwananyamala tuliamua kutumia changamoto zilizokuwa hospitalini hapa kama fursa, baada ya wizara kutuletea kifaa hiki muhimu tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kumaliza changamoto waliyokuwa wakipata ndugu wa wanawake waliojifungua ya kuja na ndoo za maji ya moto ya kuwakanda na wakati wa kuondoka tuliwabebesha kondo wakayateketeze majumbani," alisema Dk. Wambura.

Alisema sababu zilizokuwa zikiwafanya waondoke na kondo ni pindi inapotokea mashine za kuteketeza kuharibika hivyo hospitali inakosa njia mbadala ya kuyateketeza.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu wa Mwananyamala, Dk. Isdory Kiwale, alisema mashine hiyo ni ya ujazo wa gesi 308, inayoweza kutumika kupikia na kuwasha taa za hospitali.

Alisema kiasi cha gesi inayotumika kuchemsha maji ni ndogo kulinganisha na uzalishaji, hivyo wana mpango wa kutumia gesi hiyo kwa ajili ya taa za wodi ya wanawake na kutumiwa kupikia katika jiko la hospitali hiyo.

"Kutokana na kuwa gesi inayozalishwa ni nyingi na kama tulivyoeleza kwa siku wanawake 40- 60 wanajifungua ina maana tunazalisha gesi ya kutosha na hatuwezi tukaiuza nje ya hapa. Kwa siku za baadaye tunatarajia kuitumia kwa ajili ya taa za wodi za wanawake na kwenye kantini ya hospitali," alisema Dk. Kiwale.

Aidha, alisema pia wana mtambo wa kuchakata chupa na mifuko ya plastiki kutengeneza mifuko ya kuhifadhia taka za hospitali.

Alisema huduma hiyo inasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuzalisha mifuko hiyo ya kuhifadhia taka za hospitali na kupunguza gharama zisizo za lazima.

Pia alisema huduma za matibabu katika hospitali hiyo zimeimarika kutoka na kuwa na madaktari bingwa wa kutosha 24 wanaotoa huduma kwa saa 24.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**CHUO CHA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI – MBEYA)**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI (LBT)**

1. **Utangulizi:**
Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "Appropriate Technology Training Institute" (ATTI-MBEYA) ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Kozi hizi zimepangwa kufanyika kama ifuatavyo: -

| Na. | JINA LA KOZI | MUDA NA TAREHE | MAFUNZO YATAFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Kumi (10)** 06/04/2020 - 13/06/2020 | ATTI- Mbeya |
| 2 | Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana ya juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)** 18/05/2020 - 13/06/2020 | ATTI – Mbeya |
| 3 | Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji ('Bituminous surfacing of low traffic volume roads') kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)** 07/08/2020 - 12/09/2020 | ATTI – Mbeya |

2. **Masomo yatakayofundishwa: -**

(a) **Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana:** Washiriki watajifunza mada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na masomo shirikishi ambayo ni utaratibu wa kufungua kampuni kwa vikundi, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, uashi, teknolojia ya udongo na zege. Kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hususani matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent maintenance'.

(b) **Kozi ya Mafunzo ya matengenezo na ukarabati wa Barabara za Udongo/Changarawe:** Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, watajifunza juu ya: mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati. Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe/udongo kwa ubora unaotakiwa.

(c) **Kozi ya Mafunzo ya matengenezo na ukarabati wa Barabara za Lami:** Washiriki watajifunza aina za lami, aina za barabara za lami, aina za viunzi vya ujenzi wa barabara za lami (Yaani 'Bituminous road construction materials'); aina ya Vifaa na mitambo kwa kazi za ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami; kusanifu na kutengeneza tabaka la lami 'Design and construction of Surface Dressing'; kuziba viraka; kuziba mipasuko 'crack sealing'; na Usalama kazini. Lengo kuu la kozi hii ni kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kusanifu (design) na kufanya kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za lami yaani "Surface Dressing".

3. **Njia za ufundishaji**
Mafunzo yatafanyika kwa nadhalia na kivitendo.

4. **Malengo ya kozi**
Kozi hizi zimelenga kumpatia mshiriki faida na mbinu za matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika:
   i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent, Periodic and Emergency maintenance';
   ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
   iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
   iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani **"SPECIALIST LABOUR BASED CONTRACTING FIRMS"** kisha kupata sifa za kisheria za kuomba miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara inayotolewa na TARURA au TANROADS.

5. **Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**
   a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
   b) Mafundi Sanifu wa Barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
   c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi nchini,
   d) Makandarasi wenye nia ya kujenga uwezo wa kazi zao za matengenezo ya barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
   e) Watu binafsi wenye uzoefu wa kazi za barabara na wanaotaka kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

6. **Lugha ya mafunzo:-**
Kozi zote zitaendeshwa kwa kutumia lugha ya kiingereza isipokuwa kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana ambayo itaendeshwa kwa mchanganyiko wa lungha ya Kiswahili na Kiingereza.

7. **Gharama za Mafunzo: -**
Gharama ya mafunzo ni **Tshs. 500,000/=** Kwa kozi Maalumu ya Vikundi vya Wanawake na Vijana; **Tshs. 1,000,000/=** Kwa kozi ya Lami na **Tshs. 1,600,000/=** Kwa kozi ya Changarawe. Malipo ya ushiriki yalipwe kabla ya kozi kuanza kwa: **"Principal ATTI, NBC Tukuyu, A/c No.038101001741",** tunashauri yalipwe kabla ya wiki mbili na wasilisha hati ya malipo (Bank Slip) unapowasili kwenye kituo cha kozi husika.

8. **Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi: -**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi hizi wanaombwa kutuma maombi yao Chuoni ATTI – MBEYA kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizowekwa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa maelezo zaidi.

**Kumbuka:** Nafasi zilizopo ni ishirini (20) tu kwa kila kozi hivyo, tuma maombi yako mapema.

**Wasiliana nasi kupitia kwa mkuu wa chuo,**
**ATTI – Mbeya S.L.P 1957, MBEYA,**
**Simu: 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509**
**Nukushi: 025 295 7486**
**Barua pepe: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

215590502

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timu Ligi Kuu Bara ziache kwenda uwanjani na matokeo

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/2020 unatarajia kukamilika hivi karibuni, ushindani katika ligi hiyo ya juu unaendelea kuongezeka kila uchao.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali ndiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ya jijini Dar es Salaam ndio mabingwa watetezi na kwa sasa ndio vinara katika msimamo wa ligi wakati Ndanda FC ndio inayoburuza mkia.

Huku kukiwa na mabadiliko ya kanuni kuhusu idadi ya timu zinazotarajiwa kushiriki katika msimu ujao, ikiwa na maana kwamba msimu ujao wa 2020/ 21 Ligi Kuu Tanzania Bara itashirikisha timu 16 badala ya 20.

Mabadiliko hayo ya kanuni ndio yanaongeza ushindani kwa timu zote. Msimu huu kumekuwa na ushindani zaidi kwa sababu kuna klabu zinazochuana kuwania ubingwa na kuna kundi la pili la timu zinazopambana kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Hili janga la kushuka daraja ndilo linaonekana kuwa na changamoto zaidi kwa sababu idadi ya timu sita zinazotakiwa kushuka ni kubwa na katika msimamo wa ligi hiyo, klabu zimetofautiana pointi chache.

Hii inamaana kuwa ushindani katika ligi hiyo msimu huu umeongezeka na kila timu inaingia uwanjani kwa lengo moja la kupambana kuwania pointi tatu muhimu na hakuna timu inayoonekana inasindikiza klabu nyingine kama ilivyozoeleka kwa baadhi ya mechi tumeshuhudia matokeo yasiyotarajiwa.

Nipashe inafurahi kuona ligi hiyo imekuwa ngumu zaidi na kwa hali hii, inasaidia kukuza viwango vya wachezaji ambao mwisho wa siku ndio wanaitwa katika Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo Aprili mwaka huu ina kibarua cha kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Ushindani huu unaoendelea umekuwa ni sababu ya kuondoa au kumaliza 'ubabe' waliokuwa nao timu kongwe au klabu kubwa zinazotoka jijini Dar es Salaam ambazo misimu ya nyuma zilionekana zikiingia uwanjani zikiwa tayari na matokeo yao 'mfukoni'.

Hii ilizifanya baadhi ya timu kubweteka na kutofanya maandalizi ya kutosha, jambo ambalo katika msimu huu hali imebadilika kwa kila timu kutakiwa kupambana kwa dakika zote 90 za mchezo husika.


Timu zilizoko katika nafasi tano za juu bado hazina uhakika wa kutwaa taji hilo msimu huu kutokana na changamoto ya matokeo wanayoyopata sawa na klabu zilizoko katika nafasi tano za chini, na lolote linaweza kutokea.

Hali hii inasaidia kuongeza ushindani kwa kila timu kuendelea kupambana na kutoridhika na nafasi waliyopo sasa kwa sababu lolote linaweza kutokea katika mzunguko wa pili au dakika za majeruhi kama tulivyoshuhudia msimu uliopita England, Liverpool kushindwa kutwaa ubingwa kwa tofauti ya pointi moja ambayo Manchester City waliwazidi.

Hilo ndilo tunalotaka liendelee kutokea ili mashabiki waache kwenda na matokeo yao mkononi, kwa kuwa tunatambua kuimarika kwa ligi hii kutasaidia kuwatangaza wachezaji wetu kwa sababu mechi wanazocheza zinaonekana katika nchi mbalimbali kupitia king'amuzi cha Azam na pia kwa njia ya mtandao wa Youtube. Lengo letu ni kuona ligi yetu inaendelea kuvutia wachezaji wengi wa kigeni kuja kucheza nchini, jambo ambalo tunaamini siku si nyingi pia watajitokeza wawekezaji wengi katika klabu zetu na hata wadhamini.

Hivyo, tunazitaka klabu kuendelea kupambana zaidi katika kila mchezo hususan wakati huu mzunguko wa kwanza ukielekea kukamilika, ili hatimaye bingwa atakayepatikana atwae kombe hilo kwa jasho hatua itakayomfanya kuwa na uwakilishi mzuri kwenye michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga inahitaji muda, waachieni makocha

Na Adam Fungamwango

**KIPIGO** cha bao 1-0 ilichokipata Yanga dhidi ya Azam FC kimeleta mambo na maneno mengi kutoka kwa wanachama na mashabiki wa Yanga. Ni sawa tu na msiba wa 'mswahili' ambao siku zote haukosi sababu.

Hii ni baada ya mfululizo wa matokeo mabaya yanayoyapata. Ilichapwa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar, kabla ya kupigwa bao 1-0 Jumamosi iliyopita dhidi ya Azam FC. Ikumbukwe kuwa Yanga ilitoka kupata pointi moja tu, kwa kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba, hivyo mechi tatu kuambulia pointi moja tu.

Ni moja ya matokeo mabaya kwenye historia ya klabu hiyo kongwe kabisa nchini. Wanachama na mashabiki wameonekana kila mmoja kutoa lawama kivyake. Wengine wanalaumu waamuzi. Wengine wanailaumu Bodi ya Ligi. Wapo wanaomlaumu Kocha Boniface Mkwasa, sijajua kwa nini. Kuna wanaowalaumu viongozi wao kwa kubadilisha makocha mara kwa mara.

Nimemsikiliza beki wa Yanga, Juma Abdul baada ya mechi hiyo. Kusema kweli maneno aliyoongea mchezaji huyo yalipaswa kuongewa na viongozi wa Yanga.

Maneno yake yanakwepwa kuzungumzwa na viongozi wa klabu hiyo, hivyo kujipa wakati mgumu wao wenyewe mbele ya wanachama na mashabiki wao.

"Unajua sasa hivi Yanga tuko kwenye kutengeneza timu, alikuwa mwalimu Zahera (Mwinyi) alisajili wachezaji, lakini baadaye akaondoka, wakaja wachezaji wapya, tukawa na Master (Mkwasa), muda mfupi tu tukawa naye, akaja mwalimu mpya (Luc Eymael) na yeye anakuja na mifumo yake, kwa hiyo bado saa hizi mwalimu yuko kwenye kutengeneza timu," anasema mchezaji huyo na kuwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa watulivu na wavumilivu.

Haya ni maneno ambayo yana ukweli kwa asilimia nyingi na yalipaswa kutolewa na viongozi wa Yanga ili kuwapoza wanachama na mashabiki wao wasiwe na matumaini makubwa sana.

Abdul ameamua kueleza ukweli kuwa kutokana na mabadiliko haya ya kuondoa wachezaji waliosajiliwa dirisha kubwa na kusajili wengine dirisha dogo, pamoja na mabadiliko ya benchi la ufundi, bado timu haijakuwa na muunganiko.

Hicho ndiyo kinachohofiwa kuongewa na viongozi wa Yanga kwa sababu wao wamewaaminisha wanachama na mashabiki wao kuwa kwa usajili uliofanywa basi timu itatwaa ubingwa.

Ina maana kama wakisema kuwa wanatengeneza timu, wanachama na mashabiki watajua kuwa basi msimu huu hakuna ubingwa.

Na wao ndiyo watanyooshewa vidole kwa sababu walifanya usajili mwanzoni mwa msimu na kuwaaminisha kuwa wachezaji waliosajiliwa ni bora wanaoweza kutwaa ubingwa, lakini wengi wao walioonekana watakuwa muhimu kwenye timu wanaondolewa kipindi cha dirisha dogo na kuletwa wengine.

Kama ni kukosea wameshakosea, viongozi wa Yanga wanapaswa kuwaondolea tamaa ya ubingwa mashabiki wao na kuwaambia ukweli kuwa wanatengeneza timu kwa sababu wana wachezaji wengi wapya.

Hapo si tu kwamba wanawashusha presha mashabiki wao tu, lakini hata wacheaji wapya ambao wanalazimika kucheza kwa presha na wasiwasi wakati bado hawajaingia kwenye mfumo wa timu.

Sisemi kwamba Yanga haiwezi kupata ubingwa la hasha, ila presha ya ubingwa ikiondoka kwa mashabiki, makocha na wachezaji wakaachwa watengeneze mfumo na kucheza bila shinikizo, inaweza kuwasababisha kupata matokeo mazuri zaidi na hatimaye kutwaa ubingwa.

Yanga haitakiwi iishi kwa kushindana na Simba na Azam kwa sababu yenyewe imeshabadilisha wachezaji kadhaa, huku wenzao wakiwa na wachezaji wengi wale wale ambao msimu uliopita walicheza Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Mfano Simba bado ina wachezaji wengi ambao waliiwezesha timu hiyo kutinga Robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa, wakati yenyewe waliocheza Ligi ya Mabingwa msimu huu tu wameshaachwa.

Umefika wakati kwa Yanga sasa kukubali matokeo yoyote yanayopatikana na kushusha matumaini makubwa ya ubingwa kwa sababu kama alivyosema Abdul kuwa inajenga timu ambayo ni kama mpya tu kwa sasa.

Ila litakuwa ni fundisho kwa viongozi wa Yanga, isiwe tena ligi inaisha wanaacha tena wachezaji wengi na kusajili wengine wapya, badala yake kama waliopo watakidhi, basi wanatakiwa wasajili wachezaji wachache tu wa kuongezea nguvu. Vinginevyo watakuwa hawafanyi kitu, badala ya kusonga mbele wanakuwa hapo hapo tu.

## MJADALA

# Barabara Ubungo stendi iboreshwe

**Mhariri,**

*NAOMBA nitoe maoni yangu kuhusiana na kituo cha mabasi ya daladala cha Ubungo, jijini Dar es Salaam, ambayo pia inahudumia magari yaendayo maeneo jirani ya jiji la Dar es Salaam, kama Kibaha.*

*Kwanza, natoa pongezi kwa kazi nzima ya mabadiliko ya kituo hicho cha mabasi ni kizuri, hata usimamizi wake kuna askari polisi wa usalama barabarani wanaopahudumia.*

*Ila kuna tatizo kuhusu mahali panakounganisha Barabara ya Sam Nujoma, ambako ndiko mabasi mengi yanatoka na kuingia stendi.*

*Mahali hapo pako katika hali mbaya zaidi na hasa katika kipindi cha mvua kama sasa, ni shida kubwa barabara iko mbaya, maji na tope kwa wingi.*

*Nashauri, mamlaka zenye usalama nako zikachukua hatua zinazostahili kwa ajili ya kuparekebisha na kuleta tija kwa wanaohudumiwa wa pande mbalimbali za jiji, maana Ubungo Simu 200 ni kiungo cha huduma hiyo.*

*Inawezekana maoni yangu yakaangukia katika hatua hii ya awali hapo Ubungo, lakini kimsingi naenda mbali zaidi kwa vituo vyote vya daladala na barabara zake za kutokea kama ilivyo Ubungo.*


*Nitatoa mfano wa kituo kikuu cha daladala cha Segerea, ambako sehemu kubwa ya huduma za usafiri, imegeuzwa vijiwe vya wajasiriamali, baadhi hata vituo vya vibanda hivyo vimekuwa kwa ajili ya wateja wa kahawa, uji na chai.*

*Nasikitika kwamba, mamlaka ya serikali ya mtaa na wasimamizi wa kituo hicho wamebaki kimya na njia ya kutokea daladala kwenda Kinyerezi, hali ni mbaya sana.*

**Castor Edabaga, Dar es Salaam**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Samatta Aston Villa, Kichuya karudi Bongo!

**Na Adam Fungamwango**

NAKUMBUKA mwaka 2010 hadi 2011 wakati kiungo Haruna Moshi 'Boban' alipojiunga na kuicheza klabu ya Gefle IF inayocheza Ligi Kuu nchini Sweden.

Mpaka leo sijajua ni sababu gani zilizomfanya Boban arejee nchini. Kwa sababu alikuwa ni mchezaji tegemeo wa kikosi cha kwanza cha timu hiyo, pia kipenzi cha kocha.

Boban hadi leo hii anabakia kuwa ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu kuwahi kutokea nchini Tanzania.

Alirejea nchini 2011 na kujiunga na klabu yake ile ile aliyotoka ya Simba. Leo ni miaka tisa tangu Boban arejee kimaajabu kutoka nchini Sweden.

Nina uhakika kuwa kama angeendelea kukomaa kwa miaka hii tisa angekuwa mchezaji wa kwanza kucheza soka kwenye Ligi Kuu nchini England, Ufaransa, Italia, au Hispania.

Kile kipaji alichonacho, wachezaji wengi ninaowaona kwenye ligi za huko hawana. Tatizo la Boban lilikuwa ni kujitambua, kujituma, nidhamu na uvumilivu.

Wakati nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Mbwana Samatta akiwa kwenye harakati za kujiunga na klabu ya Aston Villa ya England, asingeweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza nchini Tanzania kucheza ligi hiyo. Nadhani angekuwa wa pili, kwa sababu Boban tayari angekuwa ameshapita huko.

Ukiangalia kwa jicho la kimichezo na ufundi, Boban ana kipaji kikubwa kuliko Samatta. Na pia hapa nchini kuna baadhi ya wachezaji wa Kibongo wenye uwezo mkubwa na vipaji kuliko Samatta. Lakini nahodha huyo wa Tanzania anawaacha wenzake mbali kwa suala la nidhamu, kujituma, kujitambua na uvumilivu.

Wachezaji wengi wa Kitanzania hasa wenye vipaji wanakosa vitu hivi na kusababisha waishie hapa hapa nchini na hata kama wakienda nje, baada ya miezi michache au mwaka mmoja tu wanarejea na hadithi mbalimbali zisizoeleweka vizuri.

Wapo waliorejea wakidai wamefuzu majaribio, lakini hatuoni kwenda kufanya kazi. Kuna wanaotuambia wamerudi likizo, lakini baadaye wanajiunga na klabu za hapa hapa, halafu wapo walioambiwa wakaongeze nguvu, lakini hawakuongeza badala yake wakarejea na kuongeza 'jiko' kisha kuendelea kuwa hapa hapa.

Kifupi tu ni kwamba wachezaji wa Kitanzania wanaridhika na mafanikio madogo tu ambayo wanayapata hapa, hivyo hawaoni tena umuhimu wa kujituma na kujitesa zaidi.

Wanateseka, kujituma na kujinyima wanapokuwa kwenye klabu ndogo huko mikoani, lakini wanapofika Simba, Yanga au Azam, wanapopata umaarufu, nyumba na gari, vitu ambavyo kwa utamaduni na familia zetu ndivyo muhimu kwenye maisha, wanaona hawana tena wanachohitaji zaidi, hivyo hata kwenda kucheza nje ya nchi wanaona ni kupoteza muda tu.

Hata wanapolazimika kwenda nje, maisha ya upweke ambayo hawajayazoea, mazoezi magumu ambayo wakati mwingine hawajawahi kukutana nayo hapa nchini, kila kitu kinachopangwa kinatakiwa kifanyike kwa muda mwafaka, pamoja na kulazimika kujinyima maisha ya starehe, hivi ndivyo vinakuwa mwiba mchungu kwa wachezaji wa Kitanzania, hivyo kulazimika kurejea.

Ukiangalia hata wachezaji ambao wamepambana kufika huko, Samatta na Simon Msuva ukifuatilia historia zao vizuri utajua kuwa ni wachezaji ambao hawana mambo mengi nje ya uwanja na hii inatokana na malezi waliyolelewa.

Baba wa Samatta mzee Ally Samatta akihadithia jinsi alivyokuwa akiishi na watoto wake hao, utagundua alikuwa akiwalea 'Kijerumani', yaani mzazi ambaye mtoto atafanya vile anavyotaka yeye tu basi na si mtoto anavyotaka.

Msuva amelelewa kwenye maadili ya kidini, kiasi cha hata alipoondoka kwenda nchini Morocco kucheza soka la kulipwa, alikwenda kuaga kanisani na kupewa Biblia kama mwongozo.

Hapa utagundua kuwa hawa wamefika huko kutokana na nidhamu kubwa na aina ya maisha waliokuwa wakiishi tangu wakiwa wadogo.

Nina wasiwasi mkubwa kama Tanzania inaweza kupata mbadala wa Samatta na Msuva kwa miaka ya karibuni kwa sababu kwa sasa vijana wamekuwa na nguvu mno zaidi ya wazazi wao kwenye malezi, wakiachiwa kufanya wanavyotaka kwa kisingizio cha utandawazi.

Taifa linashindwa kupata akina Samatta wengine, kwa sababu wakati mwenyewe akikaribia kutua Aston Villa, akina Shiza Kichuya, Manyika Peter wao wanarejea nchini kutoka nje.

Ina maana 'ligwaride limewashinda' na wamerudi tena hapa hapa na sina ukakika kama watatoka tena.

Kama Samatta ana miaka 27 na wataalamu wanadai kuwa alichelewa kwenda Ulaya, hawa wanaorudi watafika huko lini?

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# DC atuhumu wafanyabiashara kuhujumu miundombinu reli

**Na Godfrey Mushi,** HAI

VIGOGO wawili ambao ni wafanyabiashara wakubwa wanaotoa huduma ya usafirishaji wa abiria kati ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam, wametakiwa kujisalimisha katika Kituo cha Polisi Bomang'ombe, Wilaya ya Hai mkoni Kilimanjaro kutokana na tuhuma za kuunda genge la uhalifu na kufadhili uhujumu wa miundombinu ya reli ya Moshi-Arusha.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alitoa maelekezo hayo kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo (OCD), kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuwakamata wafanyabiashara hao, iwapo watakaidi amri ya kujisalimisha kabla ya saa 12:00 jioni ya jana.

Aliagiza hayo muda mfupi baada ya kwenda katika Kijiji cha Rundugai, kukagua miundombinu ya reli hiyo ya Moshi-Arusha inayojengwa na Wahandisi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama mliopo hapa, kama hawa wafanyabiashara (anawataja majina) hawatajisalimisha wenyewe hadi kufikia saa 10 jioni ya leo (jana), kawakamateni na kufikia saa 12:00 jioni mniletee taarifa za kwamba mmeshawakamata na wako mahabusu.

"Nimepokea taarifa kwamba hawa wafanyabiashara wa mabasi, wameunda genge la uhalifu na linahujumu miundo mbinu ya reli hii," alieleza Ole Sabaya.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, baadhi ya wahalifu wanaokwenda kuhujumu miundombinu hiyo wanaweka mawe makubwa katika njia ya reli na wengine wanachimbua chini ya reli hiyo.

Kabla ya kutoa amri hiyo, Ole Sabaya alipokea taarifa fupi kuhusu maendeleo ya ukarabati wa reli hiyo kutoka kwa msimamizi wa ubadilishaji wa njia ya reli, Sindu Singozi, alimweleza Mkuu huyo wa Wilaya kwamba kazi hiyo inaendelea vizuri licha ya kuwapo changamoto za hapa na pale.

Kwa upande wao baadhi ya wafanyakazi wanaokarabati reli hiyo, walimweleza Ole Sabaya kuwa miundombinu ya reli hiyo ilihujumiwa katika eneo la Rundugai na Kia, Wilaya ya Hai.

Alipotafutwa Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Salum Hamduni kutoa ufafanuzi kama wafanyabiashara hao wamekamatwa au kujisalimisha kwa mujibu wa amri ya Ole Sabaya, simu yake haikuwa hewani ingawa Nipashe inaendelea kumtafuta ili kutoa majibu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, akizungumza na watumishi wa iliyokuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Chalinze ( Chaliwasa), baada ya Mamlaka hiyo kukabidhiwa rasmi Dawasa. **MPIGAPICHA WETU**

## Ofisa elimu ashtakiwa wizi fedha za madawati

**INATOKA UK. 2**

kulalamikiwa kuwa mazingira ya uhamisho na upandishwaji vyeo walimu kudaiwa kugubikwa na utata.

Hatua hiyo ilifikiwa katika kikao cha madiwani baada ya kukaa kama kamati kwa mujibu wa sheria na mamlaka ya Baraza la Madiwani pale linapotaka kumjadili mtumishi, ambapo hulazimika kujigeuza kama kamati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Ali Kidwaka, alithibitisha kutolewa uamuzi huo na kwamba ulifikiwa katika kikao chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Elisha Lupuga, ambaye ndiye anayeweza kulitolea ufafanuzi zaidi suala hilo kwa kina.

Lupuga akithibitisha kuchukuliwa kwa hatua hiyo na kwamba taratibu za kuchukuliwa hatua hiyo zilizingatia kanuni na sheria katika kikao kilichofanyika Januari 6, mwaka huu.

Lupuga amesema baada ya kufikiwa uamuzi huo baraza lilimwagiza Mkurugenzi Kidwaka kumsimamisha kazi Matiku na pia kuunda kamati itakayochunguza tuhuma zinazo mkabili yakiwamo malalamiko yanayotokana na uhamisho na upandishwaji vyeo walimu kudaiwa kugubikwa na utata.

Lupuga aliongeza kuwa baada ya kamati husika kukamilisha kazi yake ya uchunguzi matokeo yake yatapelekwa mbele ya Baraza la Madiwani ambapo litatoa maamuzi kutegemeana na matokeo ya uchunguzi wa kamati hiyo bila kuonea mtu.

**Imeandikwa na Renatha Msungu, DODOMA na Renatus Masuguliko, GEITA**

# Wengi waachwa, simu kuzimwa leo

**INATOKA UK. 2**

Zubery Mohamed, mkazi wa Kahama Mjini, alisema kuwa idadi kubwa ya wananchi wameambiwa kuwa mtandano ni mbovu, hivyo zoezi hilo limekuwa likikwama mara kwa mara na kutakiwa kusubiri hadi mtandao utakapokaa vizuri.

Matias Methew alisema: "Huduma zinaenda taratibu sana hadi jana (juzi) umeme ulikatika wilayani Kahama na kusababisha huduma kusitishwa kwa siku nzima, jambo ambalo walishauri kuwa na vifaa mbadala kama jenereta ili huduma ziendelee kama kawaida ikiwa ni pamoja na kuongeza wahudumu."

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema hadi jana idadi ya wananchi waliojiandikisha kwa ajili ya kupatiwa namba ya kitambulisho cha Nida ni 296,000 kati ya wananchi 350,000 waliokusudiwa kuandikishwa na kupatiwa namba wilayani humo.

"Nimeshawaagiza Shirika la Umeme Tanzania Wilaya ya Kahama kuacha kukata umeme kwa ajili ya matengenezo ya nguzo au jambo lolote na kwamba wasubiri hadi zoezi la vitambulisho vya Nida liishe kwani zoezi hilo linategemea sana huduma ya umeme," alisema Macha.

**DODOMA**

Wakati mikoa ya Morogoro, Shinyanga ikikumbwa na kadhia hiyo, foleni za wananchi kusajili kwa njia ya alama za vidole jijini Dodoma, zilipungua huku baadhi wakiomba kutofungiwa laini zao kwa kuwa bado hawajapata namba za vitambulisho vya Taifa.

Nipashe ilitembelea eneo la Nyerere Square ambalo linatumika kusajili wananchi hao na kukuta baadhi ya wananchi wakilalamika.

Wakizungumza na gazeti hili, mmoja wa wananchi, Sesilia Pius, alisema amekamilisha kujaza fomu ya kitambulisho hicho na alipigwa picha lakini aliambiwa namba itatolewa baada ya wiki mbili ndipo ataweza kusajili laini yake kwa alama ya vidole.

"Naona namba za Nida zinachukua muda mrefu na kesho (leo) ndiyo mwisho, serikali isifunge laini itupe muda ili tukamilishe usajili kuliko kukosa mawasiliano," alisema Pius.

Asha Juma alisema alikamilisha taratibu zote, lakini ametakiwa kusubiri namba ya Nida.

Akizungumzia hatima ya wananchi hao, Meneja wa TCRA Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, alisema: "Laini zao zitazimwa hadi watakapokamilisha usajili huo na mtu ambaye laini yake itakuwa na fedha hazitatolewa hadi akamilishe usajili wake."

"Baada ya tarehe ya mwisho ya kusajili hakuna atakayepata mawasiliano mpaka atakapokamilisha taratibu za usajili kwa njia ya alama za vidole... naomba niwaambie watu kama hujakamilisha usajili hutapata mawasiliano mpaka utakapokamilisha usajili," alisema Manyanda.

Aliongeza kuwa kwa wale waliopewa muda wa kusubiri ili wapate namba inabidi wasubiri, akisema kuwa idadi kubwa ya wananchi wameshasajiliwa.

"Naiomba jamii itumie nafasi ya leo kwenda kukamilisha usajili bila kufanya hivyo watakosa mawasiliano mpaka pale watakapokamilisha usajili kwa njia ya alama za vidole," alisema Manyanda.

**DAR ES SALAAM**

Katika eneo la Chanika mwisho, idadi kubwa ya wananchi wanaotumia mitandao ya simu walishindwa kusajili laini zao kutokana na kukosa mtandao.

Wananchi wa eneo hilo jana walifika katika vituo vya usajili, lakini walishindwa kukamilisha usajili kutokana na kukosa mtandao.

Katika eneo la Kimara kulikuwapo na foleni kubwa ya wananchi waliokuwa wakisubiri kusajili laini zao, lakini hadi kufikia jioni idadi kubwa ya wananchi hao walishindwa kujisajili.

**ARUSHA**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amewakumbusha Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kuhakikisha tarehe ya mwisho iliyotolewa na Rais Magufuli inatekeleza kwa kusitisha mawasiliano ya watu watakaokuwa hawajasajili laini zao.

"Mimi nakumbusha TCRA kusimamia hili kuhakikisha muda uliotolewa wanasitisha huduma ya mawasiliano na watakaokuwa bado kusajili watafute mbinu zao za kusajili laini zao na siyo vinginevyo," alisema Gambo.

Naye Mkuu wa TCRA Kanda ya Kaskazini, Imelda Salum, alisema tangu kusogezwa kwa muda wa kusajili kuanzia Januari 6 hadi 14, mwaka huu wamesajili laini 14,161 za simu mkoani Arusha.

**Imeandikwa na Salome Kitomari, Hellen Mwango (DAR), Idda Mushi, (MOROGORO), Ndalike Sonda, (KAHAMA), Renatha Msungu (DODOMA), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA).**

# Wanawake wapewa msukumo kugombea uongozi mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MRATIBU wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) tawi la Pemba, Fat-hiya Mussa Said, amewataka wanawake kugombea nafasi za uongozi ifikapo mwaka 2020 bila kukiuka maadili.

Akizungumza katika mwendelezo wa mikutano ya kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi shehia ya Mjimbini Wilaya ya mkoani Pemba, mratibu huyo alisema kinamama wanaweza kuleta mabadiliko katika jamii, hivyo watakaposhika nafasi za uongozi nchi itapata maendeleo.

Alisema Tamwa imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inaandaa mpango mkakati wa kuwafikia wananchi mjini na vijijini ili kuwaelimisha ya umuhimu wa kuwa viongo, hivyo ni jambo la msingi kufuata maadili.

"Tamwa imekuwa ikiwasaidia kinamama katika masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, ikiwamo kuwahamasisha suala la kuingia majimboni kugombea nafasi za uongozi, ili itakapofika mwaka 2020 tuaone wamehamasika kwa wingi," alieleza mratibu huyo.

Alisema sio vyema kwa kinamama kuendelea kubaki nyuma kugombea nafasi hizo, kwani wanapowapa wanaume husababisha kukosa fursa nyingi za maendeleo na kukosa haki zao za msingi.

"Wanawake wenzangu tuacheni tamaduni zisizokuwa na maendeleo kwetu, ondoeni woga na mwondoshe dhana ya kusema mwanamke hawezi kuongoza," alisema.

Kwa upande wake Diwani wa Mtambile, Mwadini Ali Mwadini, aliwataka kinamama hao kushirikiana na kuunga nguvu za pamoja katika kumchagua kiongozi mwanamke sambamba na kuwaheshimu waume zao ili watakapogombea nafasi hizo waweze kupatiwa ruhusa kwa wepesi.

"Wanawake mna haki ya kugombea nafasi za uongozi, hivyo kuweni makini katika kuchunga ndoa zenu, ili muweze kupatiwa ruhusa," alisema.

Aliipongeza Tamwa na timu

INAENDELEA UK. 24



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza kabla ya kikao cha Bodi ya Uwekezaji ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA), kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 30 jela, viboko 12 kwa kubaka mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Matapwa, Kata ya Mipingo, Wilaya ya Lindi, Hassani Bacho Nassoro (23), amehukumiwa na Mahakama ya Mkoa huo kifungo cha miaka 30 baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa shule ya msingi mwenye umri wa miaka 14.

Mshtakiwa huyo pia amehukumiwa kucharazwa viboko 12 pamoja na kulipa fidia ya Sh. milioni moja kufuatia maumivu na majeraha aliyompatia mwanafunzi huyo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Muyonga Magala, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kama anazo sababu zitakazoishawishi Mahakama isimpatie adhabu kali kufuatia na makosa aliyoyafanya.

Hata hivyo, alidai hakulifanya kosa, hivyo kiwango cha adhabu atakachopewa anaiachia mahakama itekeleze inavyoona.

"Mheshimiwa hakimu kwa upande wangu mimi sikumbuka huyo mlalamikaji, lakini kwa vile nimeonekana nina kosa naiachia Mahakama itoe maamuzi," alidai Nassoro.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Magala alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana.

Mramba aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Hakimu Magala akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 88/2019 kupitia vifungu vya Sheria 130 (1) (2) (c) na 131 (1) kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, kwa kusema anamuhukumu kifungo cha miaka 30 gerezani.

Pia alimuhukumu kuchapwa viboko 12 matakoni, sita wakati wa kuingia gerezani na sita atakapotoka na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. 1,000,000.

Awali, Mramba alidai kuwa mshtakiwa huyo Desemba 2, 2019 asubuhi, Nassoro alimbaka mwanafunzi huyo (jina tunalihifadhi) alipokutana naye njiani wakati akienda shuleni.

Mramba aliiambia Mahakama hiyo kuwa alimsababishia maumivu na michubuko sehemu zake za siri.

# Madiwani washtukia upendeleo wa miradi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamelalamika kuwapo upendeleo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi na kuzibagua kata nyingine.

Madiwani walipaza kilio hicho kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wakichambua uchambuzi wa kupitisha bajeti ya mwaka (2020/2021), kwa mapendekezo ya makadirio ya Sh. bilioni 39, huku wakibainisha bajeti hiyo ilenge kutekeleza zaidi kwenye maeneo ambayo hayana miradi pamoja na kukamilisha miradi viporo.

Diwani wa Nsalala, Joseph Shoto, alisema kuwa kila kata kuna hitaji lake na changamoto wanazozipata wananchi takribani zote zinafanana, lakini tangu mwaka 2015 kuna baadhi ya kata zimepelekewa Sh. milioni 23, na zingine Sh. milioni 5 kutekeleza miradi iliyolengwa.

"Kwenye bajeti hii ya mwaka 2020/21, tunaomba kabisa ikawe sawa kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye kata zote, na kuacha kubagua baadhi ya kata na kupendelea kata zingine, ikiwa sote tunafanya kazi ya kuhudumia wananchi," alisema Shoto.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngasa Mboje, baada ya kuibuka kwa hoja hizo aliwataka watoe mfano ulio na uhalisia, kuwa ni kata zipi ambazo zimepewa upendeleo wa miradi ya maendeleo zaidi kuliko kata zingine.

Alisema hoja hiyo imemsikitisha ikiwa hakuna kata yoyote iliyofanyiwa upendeleo kwa kuwanyima wananchi maendeleo, na kubainisha kuwa kwenye Kata ya Tinde haijafanyiwa upendeleo. Alisema ujenzi wa kituo cha afya kwenye kata hiyo na Samuye, fedha zake ni Sh. milioni 500 zilitoka Serikali Kuu kwa maelekezo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba, alisema ameshangazwa na hoja hiyo kuwa anafanya upendeleo, na kubainisha hakuna kitu kinachofanyika nje ya bajeti iliyopangwa.

Aliwataka madiwani wajitahidi kwenye usimamizi wa ukusanyaji mapato ya ndani ili watekelezewe miradi ya maendeleo, na kuwa mpaka sasa tangu mwaka ulivyoanza wamekusanya Sh. milioni 10 tu.

# Mashirika binafsi yaonywa utegemezi

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, amesema mashirika binafsi yanapaswa kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili ili yaweze kuwafikia watu wengi zaidi na kwa muda mrefu, kuleta mabadiliko ya kudumu katika jamii.

Aliyasema hayo wakati akizindua bidhaa mpya za taulo kwa watoto wadogo, wasichana na watu wazima kutoka kwa Shirika la T-MARC Tanzania.

"Katika ulimwengu wa leo ambao fedha za wafadhili zinapungua, ni muhimu kwa mashirika kujifunza namna ya kupunguza utegemezi huu. Namna hiyo yatakuwa na uhakika wa kufikia watu wengi zaidi na kwa muda mrefu na hivyo kuleta mabadiliko ya kudumu katika jamii," alisema Mjema.

Alisema kutotegemea wafadhili kutaimarisha uwezo wa mashirika katika kutatua changamoto mbalimbali zinazolikabili taifa na kuunga juhudi za serikali kwenye kutekeleza sera ya kuifikisha nchi kwenye uchumi wa kati na viwanda.

Alisema kuzinduliwa kwa bidhaa hizo kutawasaidia wanaume na wanawake ambao wamepata changamoto mbalimbali za kiafya watakuwa wamejihakikishia afya na ustawi wao.

"Nawashukuru kwa kuja na wazo hili kwa sababu mmezingatia umuhimu wa taulo hizo na kuhakikisha kuwa zinaenda kupatikana nchi nzima. Lakini pia huduma hii inakwenda kupunguza tatizo la ukosefu wa bidhaa hizi hapa nchini," alisema Mjema.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya T-MARC, Alex Mgongolwa, alisema uzinduzi wa vidhaa hizo umelenga kutibu suala la kiafya kwa makundi husika.

Alisema lengo kuu ni kuwasaidia watu wenye umri mkubwa ambao wanakabiliwa na matatizo ya kiafya kuweza kusaidiwa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa T-MARC, Tumaini Kimasa, alisema uzinduzi wa bidhaa hizo utaleta mapinduzi nchini, utachangia katika kutoa huduma ya afya, na kuendeleza sekta ya viwanda.

# Mabaraza biashara yatakiwa kujitegemea

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya utafiti juu ya mafunzo kupigiwa mfano katika kuendesha mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya ambao umefanywa katika mikoa mbalimbali, imeishauri mikoa na wilaya kuachana na tibia ya kutegemea mno misaada kuendesha mabaraza yao.

Ripoti hiyo ambayo iliwekwa wazi kwa umma jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, hata hivyo imesifia kuwapo kwa mabaraza hayo ya biashara na kueleza kwamba ambako kuna uongozi imara wenye kuenzi ubunifu na mashirikiano, mabaraza hayo yamekuwa vichocheo muhimu vya ajenda za mipango ya maendeleo.

"Ufadhili lazima usaidie kujenga hali ya kujitegemea na uwe na sura ya kuwa endelevu vinginevyo utazaa ugonjwa wa kuwa tegemezi," ripoti hiyo imeonya mikoa na wilaya.

Wajumbe wa mabaraza hayo ni ishirini kutoka kila upande wa umma na sekta binafsi na wenyeviti ni wakuu wa mikoa na wilaya.

Ripoti hiyo imetoa mfano wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao ulitegemea sana misaada kuendesha mabaraza yake na misaada ilipotoweka mabaraza yakakwama pia.

Utafiti huo umebaini umuhimu wa mabaraza katika kutatua matatizo na kero na ripoti linatoa mfano wa Manispaa ya Morogoro. Mgogoro wa tozo kwa wafanyabiashara ulimalizwa vizuri kutokana na majadiliano baina ya wawakilishi wa manispaa na wa sekta binafsi.

Utafiti huo pia umegundua maeneo ya kupigiwa mfano. Ripoti inatoa mikoa ya Tanga, Dodoma na Kigoma. Katika Mkoa wa Tanga, ripoti inasema, mkuu wa mkoa na viongozi wa sekta binafsi wanaenzi na kusimamia kufanyika kwa mikutano ya mabaraza.

"Huu ni mfano wa kwamba kama kuna uongozi imara na utashi wa kisiasa, mabaraza yanakuwa hai na kufanyakazi vizuri," ripoti inaeleza.

Katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma, utafiti umeonyesha kwamba kwa sababu viongozi wa umma na viongozi wa sekta binafsi wanashauriana na kufanyakazi kwa karibu, matokeo yake kila wilaya katika mikoa hiyo ina eneo moja tu la kuhudumia biashara.

Changamoto ambazo zimeibuliwa na utafiti huo ni pamoja na mabaraza kutegemea mno uwepo wa mtu badala ya taasisi. Ukosefu wa fedha ni tatizo sana. Watu wenye uwezo katika sekta binafsi wanapuuza mabaraza kwa kuwa wanawasiliana moja kwa moja na wakuu wa mikoa na wilaya. Utafiti umegundua pia utokuwapo na uwelewa wa kutosha juu ya wajibu wa TNBC katika mabaraza ya mikoa na wilaya.

Utafiti huu uliagizwa na TNBC katika jitihada zake za kuimarisha mabaraza ya biashara katika ngazi ya mikoa na wilaya na umefanywa kwa ufadhili wa 'Local Investment Climate na Enabling Growth through Investment and Enterprise'.




Meneja wa Benki ya Exim tawi la Mkoa wa Iringa, Michael Richard (katikati), akikabidhi msaada wa taulo za kike kwa mlezi wa wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari ya Ruaha iliyopo mkoani humo, Fatuma Tembo (kushoto kwake), ikiwa ni sehemu ya mpango wa benki hiyo wa uwajibikaji kwa jamii unaofahamika kama Exim Cares. Wanaoshuhudia ni baadhi ya maofisa wa benki hiyo pamoja na baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 400/- kupanua zahanati kuwa kituo afya

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 400, kwa ajili ya kupanua zahanati ya kijiji cha Masinono kilichopo Kata ya Bugwema, Musoma Vijijini, mkoani Mara, ili kuwa kituo cha afya.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu jana kuwa iwapo zahanati hiyo itapanuliwa, wilaya itakuwa na vituo vitatu vya afya vinavyofanya kazi, huku juhudi za kujenga vingine zikiendelea.

Alisema, kwa sasa Musoma Vijijini ina vituo vya afya viwili vinavyofanya kazi, ambavyo amevitaja kuwa ni vya kata za Murangi na Mugango, huku vingine vikiendelea kujengwa.

"Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya upanuzi wa zahanati ya Masinono ili iwe kituo cha afya," alisema Dk. Anney.

Alisema, mpango wa serikali ni kujenga kituo cha afya kila kata unaendelea kutekelezwa, hivyo hatua ya kutoa kiasi hicho cha fedha ni mwendelezo kutimiza mpango huo, ambao unalenga kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya alisema, wilaya hiyo kwa sasa ina zaidi ya zahanati 20 zinazotoa huduma ya afya huku nyingine zikiendelea kujengwa, ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati.

"Tuna vijiji 68 na kata 21, tunaendelea kuhamasisha wananchi kuunga mkono juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo, nao wanajitolea kwa hali mali kushiriki, katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya," alisema.

Kwa upande wake Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, amewaomba wakazi wa Kata ya Bugwema wajitume, washirikiane ipasavyo ili upanuzi huo ukamikike mapema.

"Ndugu zangu wa Kata ya Bugwema, fursa imepatikana, naomba tujitume na tushirikiane ipasavyo, ili ujenzi ukamilike kabla ya Mei 30, mwaka huu...hongera Kata ya Bugwema," Prof. Muhongo alisema.

Aliongeza kusema: "Ushauri wangu ni kwamba wananchi tuchangie ujenzi huo ili fedha zilizotolewa na serikali ziweze kutupatia majengo mengi muhimu ikiwamo jengo la chumba cha kuhifadhia maiti."

Alisema, wakazi wa kata hiyo wamekuwa wakihifadhi maiti, katika chumba katika Kituo cha Afya cha Nyamuswa, Ikizu wilayani Bunda, na kwamba muda umewadia wa kujenga chumba hicho kijijini Masinono.

"Tuendelee kujenga na kuboresha miundombinu ya afya jimboni mwetu kwa kushirikiana na serikali yetu ili tusonge mbele na ikiwezekana, ujenzi wa kituo hicho ikamilike kabla ya Mei 30 mwaka huu," alisema.

Prof. Muhongo alisema, ushauri alioutoa wa kukamilisha upanuzi wa zahanati hiyo kabla ya Mei 30, ni kutaka kuwahi mwaka wa fedha wa serikali, ambao unaishia Juni 30.

Aliongeza kusema, zahanati ya kijiji cha Masinono ina gari la kubebea wagonjwa lililotolewa na yeye mwenyewe, na anafurahi kuona serikali ikitoa fedha za kupanua zahanati hiyo kuwa kituo cha afya.

# Kampuni uwindaji Green yatakiwa kukabidhi kitalu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
LONGIDO

KAMPUNI ya uwindaji ya Green Miles imetakiwa kukabidhi kitalu cha uwindaji ilichokuwa inamiliki awali cha Lake Natron (East) kilichopo Wilaya ya Longido mkoani Arusha ifikapo Januari 20 mwaka huu.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Frank Mwaisumbe, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji cha Mundarara na kueleza kuwa Green Miles inatakiwa kuikabidhi serikali kitalu hicho kwa amani.

Mwaisumbe alisema kampuni hiyo ilitakiwa kuondoka katika kitalu hicho tangu Desemba 16, mwaka jana, lakini waliomba kuongezewa muda ili wakamilishe uwindaji na kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii iliwakubalia ombi lao.

Alisema baada ya muda waliomba kuongezewa kumalizika, kampuni hiyo iliendelea kukaa katika eneo hilo, na serikali imeshawapa barua nyingine ya agizo la kuondoka kupitia kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda.

"Barua hiyo inaitaka kampuni hiyo na mwekezaji ifikapo Januari 20 wawe wameshaondoka katika eneo hilo na kukabidhi kitalu kwa serikali," alisema Mwaisumbe.

Naye Diwani wa Kata ya Mundarara, Alais Mushao, aliipongeza serikali kwa kumwondoa mwekezaji huyo. Alisema mwekezaji huyo hakuwa na mahusiano mazuri na wananchi wa vijiji vinavyozunguka kitalu hicho.

"Tangu aanze uwindaji katika eneo hili mwaka 2013, hajalipa malimbikizo ya tozo ya Sh. milioni 350 kwa serikali na vijiji vinavyozunguka eneo la kitalu," alisema Mushao.

Mkazi wa Kijiji cha Mundarara, Julius Malulu, alisema kampuni hiyo imekuwa haina mahusiano na vijiji ikiwapo kushindwa kulipa tozo mbalimbali.

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Longido, Michael Laizer, alimpongeza Rais John Magufuli kwa uamuzi wa kuiondoa kampuni hiyo ya uwindaji.

"Tunampongeza Rais Magufuli, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mkuu wa Mkoa Arusha na Mkuu wa Wilaya kwa uamuzi huu wa kuiondoa kampuni hii, ambayo imekuwa kero kwa wananchi," alisema Laizer.

Agosti 7, mwaka jana Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, alitangaza kuiondoa kampuni hiyo katika kitalu hicho ambacho kimekuwa na migogoro baina ya kampuni hiyo na wananchi wa vijiji 23 vinavyozunguka kitalu hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Longido na Mkoa wa Arusha.



Msanii wa uchongaji kutoka Zimbabwe, Sikulize Banda, akiwa anaonyesha waandishi wa habari namna anavyochonga mti wa mringaringa na kutengeneza vinyago vya wanawake mashujaa. Alisema aliamua kuchonga mwanamke kwa sababu hakuna nchi inayoendelea bila ya mwanamke, huku akibainisha ni kumbukumbu na mafunzo kwa vizazi vijavyo na watu watakaohudhuria Tamasha la Kan Festival linalotarajia kufanyika Januari 24 na 25, mwaka huu jijini Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ukusanyaji mapato madini ya ujenzi waipaisha halmashauri

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imejigamba kuvuka lengo la ukusanyaji mapato yanayotokana na madini ya ujenzi.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Mboje Makeleja, alisema hadi sasa wameshakusanya Sh. milioni 9.16, lengo kuu likiwa ni kukusanya Sh. milioni 3.2 kutoka kwenye madini ya ujenzi.

"Ukweli tunanufaika kwa kiasi kikubwa sana, na sasa hivi tunakwenda vizuri na ukusanyaji wa mapato yetu yamepanda tangu tuanze kukusanya kutoka kwenye madini haya," alisema Makeleja.

Alisema wamefanikiwa kuvuka lengo la ukusanyaji mapato baada ya kumweka mtu ambaye anakusanya fedha zitokanazo na madini hayo.

Alisema tani moja hadi saba ya ushuru wa madini hayo ni Sh. 5,000 kwa safari moja ya gari, na tani nane na kuendelea ni Sh. 10,000.

"Kutokana na mafanikio hayo mwaka wa fedha 2020/2021 tumeongeza malengo tunatarajia kukusanya Sh.milioni 18, mwanzoni tulikuwa kwenye majaribio sasa hivi hakuna utata wowote kupitia sheria zetu za mapato ya ndani tunawabana," alisema Makeleja.

Alisema kwa mtu anayekaidi kulipia ushuru anatozwa faini ya Sh. 200,000.

Mkazi wa Babati, John Thomas, akizungumza na Nipashe alisema halmashauri kutoza ushuru huo ni jambo zuri kwa sababu wenye magari wanapata kipato kikubwa.

# Kamwelwe ataka wananchi kuchangamkia fursa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imewataka wananchi kuchangamkia fursa za ajira kwenye ujenzi wa jengo la makao makuu ya Posta Afrika (PAPU) lililoanza kujengwa mkoani Arusha Januari mwaka huu.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa ujenzi wa jengo la makao makuu hayo.

Waziri Kamwelwe alisema jiwe hilo limewekwa Siku ya Maadhimisho ya Miaka 40 ya Uanzishwaji wa Umoja huo, ikiwa ni sehemu ya kuenzi jitihada na fikra za Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere aliyetoa eneo hilo.

"Mradi huu ni mkubwa na wa gharama kubwa na utekelezaji wake unafanyika nchini, watalaamu wengi watahitajika, natoa wito kwa Watanzania kuchangamkia ajira pindi zitakapotokea na watakaoajiriwa wawe waadilifu katika utendaji kazi ili mwisho wa siku tupate jengo lenye ubora sawa na thamani ya fedha iliyotumika," alisema Kamwelwe. Alisema jengo hilo litakapokamilika litatumika kama kitega uchumi na kwamba shughuli mbalimbali za kiuchumi na kibiashara zitafanyika na litakuza uchumi wa nchi.

"Jengo hili kwa Arusha litatoa ajira na kuboresha mandhari ya Jiji, pia litadumisha heshima ya nchi yetu mbele ya wanachama wa Umoja huu duniani kote," alisema Kamwelwe.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi James Kilaba, alisema ujenzi huo ni matokeo ya makubaliano kati ya TCRA kutoa asilimia 40 na PAPU asilimia 60 kwa kuingia ubia wa kujenga makao makuu hayo.

Mtendaji Mkuu wa PAPU, Bishar Hussein alisema jengo hilo, litakapokamilika kutaanzishwa Chuo cha Mafunzo Arusha ili kutoa fursa zaidi kwa Watanzania.

Mkataba wa mradi wa ujenzi huo, ulisainiwa Desemba 23, mwaka jana na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 33.58, utatekelezwa kwa ubia kati ya serikali kupitia TCRA na (PAPU)na litakamilika baada ya miezi 30.





## Uchunguzi uhujumu bwawa kitendawili

**Na Godfrey Mushi,** SAME

UCHUNGUZI dhidi ya watu wanaodaiwa kuhujumu mradi wa Bwawa la umwagiliaji la Kalimawe liliopo Wilaya ya Same, bado ni kitendawili.

Wanaochunguzwa kuhusiana na sakata hilo ni pamoja na viongozi wa serikali ngazi ya kijiji.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema bado vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi wake, licha ya viongozi hao kupewa nafasi nyingine ya kutubu hadharani na kisha kuirejesha mitambo ya kufua umeme wa jua iliyochukuliwa kiutata.

Watu hao wanadaiwa kuing'oa mitambo hiyo na kuiondoa eneo hilo. Watu wanaodaiwa kuwa viongozi wa umma wakishirikiana na baadhi ya wananchi katika Kijiji cha Karamba, Kata ya Kalimawe, waling'oa mitambo hiyo iliyokuwa ikitumika kusukuma maji. "Nyie viongozi wa Karamba na wengine mnaojua mmeshiriki kuukwamisha mradi huu wa umwagiliaji, rejesheni solar zilizokuwa zinatumika kusukuma mitambo ya maji. Baada ya siku 30 kupita, nitalia na nyie.

"Suala la kurejesha solar hizo ni agizo la waziri, naomba sana msimchonganishe waziri, serikali na wananchi wake."

Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka wakazi Karamba kuheshimu na kuendelea kushirikiana na vijiji vingine vinavyolizunguka Bwawa la Kalimawe vinavyotekeleza mradi wa kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mwaka jana, vijiji vinne viliingia makubaliano ya ubia katika uwekezaji huo na Kampuni ya Norway na ile ya Mikono Tayari ya Tanzania.

Kampuni hizo zimeahidi kujenga kiwanda cha kisasa cha kusindika minofu ya samaki kwa ajili ya soko la ndani na la kimataifa.

Bwawa hilo lenye urefu wa mita 4,000 na upana wa mita 5,000 lilijengwa na serikali ya wakoloni, kati ya mwaka 1952 na 1959.

# Mghwira aonya TRA mapato mbio za nyika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewaonya maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa, kuacha kukadiria mapato ambayo hayamo katika mashindano ya mbio za nyika za Kilimanjaro Preumium Lager Marathon 2020.

Badala yake, ametaka mamlaka hiyo ishiriki moja kwa moja kuanzia maandalizi ili kila mtu afahamu thamani na gharama ya maandalizi ya aina hiyo ya michezo. Mghwira alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wafanyabiashara, wawekezaji na wadau mbalimbali wa michezo kutoka ndani na nje ya nchi walioshiriki uzinduzi wa maandalizi ya mashindano ya mbio za nyika za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi mwaka huu katika mji wa kitalii wa Moshi.

"Mdau namba moja ambaye ni TRA (Mamlaka ya Mapato), niombe sana mwaka huu tushiriki kikamilifu, tuanze kushiriki kuanzia sasa kwenye maandalizi ili kila mtu afahamu thamani na gharama ya maandalizi ya aina hii. Msikadirie mambo ambayo hayapo, pia tusiache mambo ambayo tunatakiwa kuyafanya.

"Kwa hiyo, kwa kuanzia na huyu mdau namba moja ambaye nadhani ndiye anayenifuata hapa (Meneja Msaidizi wa TRA mkoa wa Kilimanjaro, Khaled Mchuma), namuomba na yeye mwaka huu adhamini mbio mojawapo, ndio ushiriki kamili huu wa TRA."

Kabla ya kuzindua maandalizi ya mbio hizo Dk. Mghwira alieleza hisia zake kuhusu ushiriki mdogo wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambazo zinawajibu wa kuwapo katika maandalizi hadi siku ya mashindano hayo.

"Na hapa naomba niongeze, wadau ambao ni waandaaji wawafuate Wizara ya Maliasili na Utalii, sisi wadau tunamletea yeye wateja, tunamletea mapato, tunamletea kila kitu halafu hatumwoni yeye akikaa na sisi akitembea na sisi.

Aliendelea: "Hata katika tukio kama hili tulitakiwa tuwe na mwakilishi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na tuwe na mwakilishi kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Lakini kwa kweli tuombe sana wizara hii kupitia idara zake nyingine za Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (Kinapa) na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) pamoja na hifadhi nyingine waje kudhamini tukio hili na litapata sura kubwa na nzuri kitaifa na kimataifa."

Alitaka udhamini wa hifadhi zilizoko chini ya Tanapa pamoja na taasisi nyingine za uhifadhi duniani zinazojishughulisha na masuala ya utalii, zichangamkie fursa hiyo lakini ni lazima waandaaji waihusishe ofisi yake.

Alisema mkoa huo unapata heshima kubwa na faida kubwa inarudi kwao na inawafanya watu wa Kilimanjaro kuwa kama mkoa wa kimataifa, kwa sababu wamezoea kupokea wageni kupitia utalii, lakini wageni wengi kupitia Kili Marathon na maonyesho ya kimataifa ya utalii ya Karibu Kili Fair, ambayo yote yanaleta watu wengi na bado kuna kuwa na matukio mengi katikati ya mwaka ambayo yanawaweka karibu na dunia.



Mwakilishi wa Kampuni ya Bico Engineering akimwonyesha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela (wa pili kushoto), eneo la uchimbaji wa kuongeza kina cha bahari katika Bandari ya Tanga. Kina hicho kitasaidia kuongeza ufanisi wa bandari hiyo ambapo meli kubwa za mizigo zitakuwa na uwezo wa kutia nanga moja kwa moja kwenye gati. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Agizo la Mbarawa mita za maji latekelezwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (Muwsa), imeanza kutekeleza agizo la Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, la kufunga mita za maji za malipo kabla (prepaid) katika makazi ya watu na taasisi za umma.

Jana, Kaimu Meneja wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph, alieleza hayo wakati wa mahojiano maalum na Nipashe kuhusu mikakati yake ya kupambana na wadaiwa sugu wa ankara za maji.

"Ni kweli tumeshaanza kutekeleza agizo la Waziri wa Maji la kufunga mita za prepaid (mita za maji za malipo kabla) kwa wateja wapya na kimsingi tumeshaanza utekelezaji wake katika makazi ya watu na taasisi zote za umma. Tunafanya hivyo ili kuwadhibiti wadaiwa sugu wasiendelee kuitia hasara mamlaka," alisema.

Kwa mujibu wa mhandisi huyo, taasisi za umma zilizofungiwa mita hizo ni pamoja na Jeshi la Polisi, Magereza na Shule ya Polisi Moshi (MPS).

Hadi sasa, taasisi za umma mkoani Kilimanjaro ikiwamo Jeshi la Polisi, Magereza na Shule ya Polisi Moshi wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 2.3.

Mhandisi huyo alisema, kufungwa kwa mita za maji za malipo kabla zitasaidia kudhibiti madeni sugu ambayo yamekuwa yakikwamisha mamlaka hiyo kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Alisema kwa sasa itaanza kuwafungia mita za maji za malipo kabla kwa kila nyumba ya askari polisi, badala ya kutumia mita moja ambayo pia ilikuwa ikitumiwa na ngome kuu na hivyo kufanya matumizi kuwa makubwa zaidi, na hivyo ngome kushindwa kusitishiwa huduma pale deni linapozidi kuwa kubwa.

Aidha, Mhandisi Aron alisema Muwsa imeshapata mita za malipo kabla zipatazo 97 ambazo zitafungwa katika taasisi za umma.

Alisema lengo la zoezi hilo ni kuhakikisha Muwsa haiendelei kulimbikiza madeni kwa taasisi za umma na makazi ya kila askari na kwamba pamoja na kufunga mita hizo, madeni yote ya nyuma wanayodai taasisi yatapaswa kulipwa na taasisi husika.

Aidha, Ofisa Uhusiano wa Muwsa, Rashid Nachani, alisema mamlaka hiyo pia inakusudia kuanza zoezi la kuzijengea chemba zote za maji zilizopo mjini Moshi ili kuongeza usalama kwa watumia huduma ya maji, kwa kuwa chemba nyingi ni chakavu hazina vifuniko.

"Tunakuja na utaratibu wa kujenga chemba maalumu kuwa za aina moja na tutazijenga katika maeneo sahihi kwani nyingi zilijengwa katika maeneo siyo sahihi na kuzifungia ufuniko kwa ajili ya kuimarisha usalama," alisema Rashid.

Nipashe Spotika



REKODI 3 ZA RONALDO ZINAZOMTESA MESSI UK. 20



## ISIKUPITE

WAKATI ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Crystal Palace juzi, Pep Guardiola alikuwa kocha wa tano kuiongoza Manchester City kwenye mechi ya Ligi Kuu katika siku yake ya kuzaliwa, na makocha wote watano waliofanya hivyo washindwa kuibuka na ushindi (pia Brian Horton mwaka 1995, Joe Royle mwaka 2001, Mark Hughes mwaka 2009 na Roberto Mancini mwaka 2010 na 2011).

# BAKORA...

Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Martinelli, akiachia shuti langoni mwa Sheffield United wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Emirates juzi. **PICHA: MTANDAO**

SOKA

# ARTETA ALIPOIPATIA ARSENAL NI HAPA




**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekuwa kocha wa Arsenal katika mechi sita tu hadi sasa, lakini tayari timu imeonyesha kuimarika. Raia huyo wa Hispania ameshinda mechi mbili, sare tatu na kupoteza mchezo mmoja, lakini katika mechi zote hizo, 'Washika Bunduki' hao wameonyesha ubora wa kiwango chao.

**Hivyo, matokeo yake yanaweza kubadilika kwenye kikosi hicho, kwani klabu sasa inaonyesha inacheza kwa kuelewana.**

Hapa tunaangalia maeneo manne ambayo tayari yameonyesha kuimarika kwa Arsenal chini ya Arteta, yafahamu...

### 4. MASHUTI MACHACHE LANGONI MWAO

Chini ya Unai Emery, kitu kilichokuwa kinaogopesha ni idadi ya mashuti ya timu waliyokuwa wanapata kwenye mchezo mmoja. Washika Bunduki hao walikuwa wanaingia kwenye mchezo wakionekana kuwa timu dhaifu zaidi na walikuwa wanapiga mashuti machache zaidi kwenye mchezo. Timu pinzani ilikuwa inashambulia zaidi lango la Arsenal na kupiga mashuti mengi zaidi.

Kama unakabiliwa na timu ambayo inapiga mashuti mengi zaidi langoni mwako maana yake unaongeza nafasi ya kuruhusu kufungwa mabao. Bila shaka safu ya ulinzi ya Arsenal haina ule ubora unaotakiwa.

Katika mechi tano za mwisho za Emery, Arsenal iliruhusu wastani wa nafasi 12.8 na kupigiwa mashuti 17.6 kwa mchezo mmoja. Kwa upande mwingine katika kipindi cha wiki tatu, Arteta amepunguza idadi hiyo hadi wastani wa 8.6 na mashuti 11.8 kwenye mchezo mmoja. Kama Arsenal itaweza kupunguza idadi ya mashambulizi kuelekea kwenye lango lake, itaweza kuutawala mchezo.

### 3. NAFASI NYINGI ZIMETENGENEZWA

Kutengeneza nafasi ni kitu ambacho Arsenal ilikuwa ikikabiliana nacho na kuonekana kigumu zaidi msimu huu. Ukweli ni kwamba kama Pierre Emerick-Aubameyang hafungi, hakuna mwingine aliyekuwa anafanya hivyo. Timu ya Emery ilikuwa inamtegemea zaidi mshambuliaji huyo raia wa Gabon.

Katika mechi tano za mwisho za Emery, Arsenal ilitengeneza wastani wa nafasi 7.2 kwa mchezo mmoja. Na katika mechi tano za kwanza za Arteta, ikatengeneza wastani wa nafasi 8.2 kwa mchezo mmoja.

### 2. UMILIKI WA MPIRA WENYE MAANA

Kipindi chake, Emery alibainisha kwamba falsafa yake ya kimchezo ni kumiliki zaidi mpira. Lakini kitu alichosahau ni kwamba kumiliki mpira bila kutengeneza nafasi ya kufunga ni sawa na bure.

Tangu kuja kwa Arteta Arsenal, hawajacheza kwa kumiliki mpira zaidi, lakini wamecheza asilimia 30 za pasi zake kwenda mbele. Emery alikuwa na wastani wa kumiliki mpira kwa asilimia 58.26 katika mechi zake tano za mwisho, lakini hakushinda hata mmoja, wakati Arteta wastani wake ni asilimia 50.15% na hajafungwa kwenye mechi nne kati ya tano kwenye mchezo mmoja.

### 1. KUSHAMBULIA

Chini ya Arsene Wenger, Arsenal ilikuwa inacheza kwa staili ya kushambulia kwa kasi na ilikuwa mbinu yao nzuri zaidi kwa kipindi cha miaka michache iliyopita. Lakini Emery aliichezesha timu na kuonekana ikishambulia polepole zaidi na hivyo kujikuta ikiruhusu zaidi mashambulizi langoni mwake.

Lakini Arteta ameweza kuanzisha staili yake ya kushambulia na kumiliki mpira, kitu ambacho Arsenal ilikuwa haina. Falsafa ya Arteta imeifanya Arsenal sasa kutengeneza nafasi kutoka kona zote hasa kwa kumruhusu Mesut Ozil kucheza kwa staili yake ya kupanda na kusaidia mashambulizi.

**JE, WAJUA?**

WATFORD ndiyo timu pekee Ligi Kuu England ambayo imecheza mechi nyingi (8) za ligi bila kuruhusu bao msimu huu. 'Hornets' hao ndiyo wanaoongoza kwa kucheza mechi nyingi (11) za ligi bila kufunga bao.



## MICHEZO



# WA DIRISHA DOGO WALIOANZA KUTISHA

Straika mpya wa Yanga aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, Tariq Seif akinyoosha mikono juu kuomba radhi kutokana na kuifunga timu yake ya zamani ya Biashara United. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

KIPINDI cha dirisha dogo la usajili kilimalizika Januari 15 mwaka huu, kilichoanza tangu Desemba 15, mwaka jana.

**Kilikuwa ni kipindi cha klabu kusajili wachezaji watakaoonekana kuziba mapengo yaliyojitokeza kwenye mechi zilizokwishachezwa msimu huu.**

Baadhi ya wachezaji waliosajiliwa kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili wameanza kuonyesha cheche katika mechi zao za mwanzo tu za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hii inaonekana kuwa baadhi ya timu hazikufanya makosa kuongeza wachezaji kipindi hiki na pia zimeziba mapungufu ambayo timu zao zilikuwa nayo.

Ikumbukwe kuwa msimu huu wachezaji waliokuwa wakisajiliwa hawakusubiri pingamizi kama misimu ya nyuma, bali walicheza moja kwa moja pale usajili wake ulipokamilika.

Hawa ndiyo baadhi ya wachezaji waliosajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo, lakini wameanza kwa kuuwasha moto kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara...

**1. TARIQ SEIF- (YANGA)**

Tariq Seif, straika mpya wa Yanga, aliyesajiliwa dirisha dogo kutoka Misri, lakini akiwa ni mchezaji wa zamani wa Stand United na Biashara United, aliifungia timu yake mpya bao Desemba 30, mwaka jana, akiifunga timu yake ya zamani Biashara United, Yanga ikishinda bao 1-0.

Ilikuwa ni dakika ya 84 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, akiingia kipindi cha pili na kufunga bao pekee, ikiwa ni siku 15 tangu kipindi cha usajili kianze.

**2. EDSON KATANGA- (JKT TANZANIA)**

Ni straika aliyesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo akitokea Green Warriors, timu inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Tayari Katanga ameshafunga mabao mawili kwa muda mfupi, kwani Januari 3 alifunga bao pekee kwenye mechi ambayo timu iliyomsajili JKT Tanzania ikishinda 1-0 dhidi ya Ndanda na akafunga lingine siku tano baadaye katika Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza, JKT Tanzania ikiitwanga Alliance FC 1-0.

**3. KELVIN SABATO- (KAGERA SUGAR)**

Huyu ni straika mzoefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Kelvin Sabato amesajiliwa na Kagera Sugar kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo akitokea klabu ya daraja la kwanza, Gwambina FC, lakini kipindi kifupi tu, amefunga bao katika mechi iliyochezwa Januari 11 dhidi ya Polisi Tanzania.

Licha ya timu yake kuchapwa mabao 2-1, lakini straika huyo wa zamani wa klabu za Ndanda, Mtibwa Sugar na Stand United, alifunga bao la kufutia machozi na kwenye mechi dhidi ya Yanga, Kagera ikishinda mabao 3-0 alitoa mchango mkubwa.

**4. ENOCK MKANGA- (MWADUI FC)**

Kwa muda mfupi tu aliosajiliwa na Mwadui FC ameonyesha atakuwa mwiba mchungu kwenye Ligi Kuu kwani tayari ameshapachika mabao mawili katika nyavu za timu pinzani.

Desemba 31, mwaka jana kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, alifunga bao timu yake ikitoka sare ya 1-1 dhidi ya KMC, lakini kwenye uwanja huo huo, Januari 8, mwaka huu, akafunga tena bao likiisaidia Mwadui FC kutoka sare nyingine nyumbani dhidi ya Ruvu Shooting.

**5. KELVIN FRIDAY- (BIASHARA UNITED)**

Ni mchezaji aliyezunguka klabu nyingi, ikiwamo Azam FC, Mtibwa Sugar na nyingine nyingi, lakini kwa sasa amejiunga na klabu ya Biashara United kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo.

Januari 11 kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Kelvin Friday alisawazisha bao dakika ya 90 na kuinusuru Biashara United na kipigo kutoka kwa Coastal Union.

Ilikuwa ni baada ya Ayoub Lyanga kuipatia bao Coastal Union dakika ya 50, lakini kijana huyo aliyesajiliwa dirisha dogo alisawazisha dakika za mwisho na kuifanya mechi hiyo kuisha kwa sare ya bao 1-1, ikihitimisha ushindi wa mechi sita mfululizo iliokuwa imeupata Coastal Union kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**NJE YA UWANJA**

MECHI dhidi ya Crystal Palace juzi, ilikuwa ni ya 300 kwa David Silva kuichezea Manchester City kwenye Ligi Kuu, hivyo kuwa mchezaji wa kwanza katika klabu hiyo kuweza kufikisha idadi hiyo kwenye mashindano hayo.



Extra Time

# TIMU 5 ZINAZOWEZA KUWEKA REKODI HATUA 16-BORA UEFA



Liverpool wakisherehekea ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita. **PICHA: MTANDAO**

**NYON,** Uswisi

MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya timu 16-bora, ratiba yake imepangwa kufanyika Februari 2020. Timu sita zilifuzu kwa hatua hiyo msimu huu kwa kutofungwa kwenye hatua ya makundi.

**Miongoni mwa timu zilizokuwa washindi wa kundi walikuwa Bayern Munich, ambayo ilikuwa ni timu ya sita katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kushinda mechi zote za makundi.**

'Wakuja' kwenye ligi hiyo wakicheza kwa mara ya kwanza, Atalanta kutoka Ligi Kuu ya Italia, Serie A, ilikuwa timu ya kwanza kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kupoteza mechi zake tatu za kwanza.

Wakati huo huo, bingwa mara tatu ambaye msimu uliopita alifuzu kucheza nusu fainali, Ajax ilishindwa kuvuka hatua ya makundi baada ya kipigo cha mechi yake ya mwisho kutoka kwa Valencia na kutupwa kule Ligi ya Europa.

Kwa upande mwingine, hapa tunaangalia rekodi za timu tano ambazo zinaweza kuzifikia kwenye hatua hiyo ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, twende sasa...

### 1. REAL MADRID KUWA TIMU YA KWANZA KUCHEZA MECHI 100

Real Madrid ni mabingwa wenye rekodi ya kulitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara 13 na walitinga hatua ya mtoano kwa ushindi wa rekodi ya mechi 23 mfululizo. Ni timu pekee ambayo imefuzu hatua ya pili ya mtoano ya mashindano hayo kila mwaka kwa kipindi cha karne moja.

Bila mshangao, imecheza jumla ya mechi 95 katika hatua hiyo tangu kuanzia msimu wa 2003-04.

Miamba hao wa Hispania kama watafuzu kucheza nusu fainali tangu wanyakue taji hilo msimu wa 2017-18, watakuwa timu ya kwanza kucheza mechi 100 kwenye hatua ya mtoano.

### 2. BARCELONA, BAYERN ZINAWEZA KUSHINDA MECHI 50 HATUA YA MTOANO

Barcelona ambayo imeshinda mechi 47 hatua ya mtoano, inaweza kufikisha mechi 50 kushinda kwenye hatua hiyo ya mashindano hayo. Miamba hao wa Catalunya pia wanaweza kufuzu kucheza robo fainali au nusu fainali ya michuano hiyo msimu huu.

Nao Bayern Munich ambao wameshinda mechi 44 kwenye hatua hiyo, wanaweza kufikisha ushindi wa mechi 50 kwa hatua hiyo. Bayern pia inaweza kuweka hitoria ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao kwenye hatua hiyo.

### 3. JUVENTUS INAWEZA KUFUNGA MABAO 100 HATUA YA MTOANO

Ni timu tatu tu - Real Madrid (166), Bayern Munich (164) na Barcelona (159) - ambazo zimefunga mabao zaidi ya 100 kwenye hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sasa msimu huu Juventus inaweza kuwa timu ya nne kufikia hatua ya kufunga mabao hayo. Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Italia, Juventus wamefunga mabao 92 kwenye hatua ya mtoano.

Bianconeri hao wanahitaji kufunga mabao nane kwenye hatua hiyo msimu huu ili kuwa timu pekee ya nne kufikisha mabao 100 kwenye hatua ya mtoano wa michuano hiyo.

### 4. LIVERPOOL INAWEZA KUWA TIMU YA PILI KUTETEA TAJI

Real Madrid ilikuwa timu ya kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kushinda taji hilo mara mbili mfululizo miaka michache iliyopita. Wakati huo akiwa bingwa mtetezi, walimfunga Juventus msimu wa 2016-17 kwenye fainali na kulitwaa taji hilo kwa mara ya 12 kwenye historia yao.

Liverpool kwa sasa ndio bingwa mtetezi wa michuano hiyo, huku wakiwa na rekodi nzuri ya kushinda mechi 20 kati ya 21 kwenye Ligi Kuu msimu huu 2019-20 kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Manchester United. Wekundu hao wanaweza kutawala pia Ulaya kama ambavyo kwa sasa wanatawala Ligi Kuu ya England. Na itakuwa timu ya kwanza kutoka England kulitwaa taji hilo mara mbili fululizo.

### 5. ATALANTA WANAWEZA KUSHINDA KWA MARA YA KWANZA HATUA YA MTOANO

Timu pekee ambayo inacheza kwa mara ya kwanza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu ni Atalanta. Na imekuwa timu ya kwanza kwenye historia ya michuano hiyo kufuzu hatua ya mtoano baada ya kupoteza mechi zake tatu za kwanza kwenye hatua ya makundi.

Huku ikiwa na msimu mzuri uliopita kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, pia inaweza kuwa timu ya kwanza kupata ushindi kwenye hatua ya mtoano wa michuano hiyo baada ya Leicester City msimu wa 2016-17.

## Nukuu

"Kwa uhakika inatia hasira kufikiria kwamba kuna mtu ameshinda Ballon d'Or nyingi kuliko yeye [Ronaldo], ningependa kumsaidia kwanza Cristiano kushinda Ballon d'Or ya sita," **Kocha wa Juventus, Maurizio Sarri akionyesha kukerwa na kitendo cha Lionel Messi kutwaa Ballon d'Or mara nyingi zaidi kuliko nyota, Cristiano Ronaldo.**



"Kumsajili Ibrahimovic kwa hakika limekuwa jambo muhimu sana, kwa uhakika ni jambo muhimu kwa upande wetu, kuliko kile anachokifanya kila siku dimbani. Ibra atatuimarisha sisi kufikia malengo yetu. Ni mchezaji wa kiwango cha juu anaweza kuisaidia timu kwa sababu anafunga mabao mazuri na ya muhimu kwa upande wetu," **Kocha wa AC Milan, Stefano Pioli akiufurahia usajili wa Zlatan Ibrahimovic.**



"Mauro anafanya kazi na sisi, akicheza kwa staili nzuri na nidhamu ya hali ya juu pamoja na wachezaji wenzake jambo ambalo ni muhimu kwetu. Sasa hajafunga katika mechi zake mbili zilizopita, lakini anacheza kwa nidhamu ya hali ya juu. Lilikuwa jambo muhimu na kuvutia. Sina shaka na Mauro," **Kocha wa PSG, Thomas Tuchel akikunwa na ubora wa Mauro Icardi baada ya Paris Saint-Germain kupata ushindi mtamu dhidi ya Monaco, Jumatano iliyopita.**





Beki wa Yanga, Ally Mtoni Sonso (kulia), akiwa na wachezaji wenzake. Jumamosi iliyopita alijifunga bao.

# WAKUJIFUNGA KAMA SONSO LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Ally Mtoni Sonso alijifunga bao dakika ya 25 kwenye mechi ya Ligi Kuu Jumamosi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam dhidi ya Azam FC.

**Bahati mbaya sana kwake, hilo likawa bao pekee kwenye mchezo huo na lililoamua mchezo, Azam ikishinda 1-0.**

Ilikuwa patashika kwenye lango la Yanga, Farouk Shikalo akaupangua mpira ambao ulikwenda kumgonga beki huyo na kurejea tena nyuma, kabla ya kujaa nyavuni.

Ilikuwa ni siku mbaya kwa beki huyo aliyesajiliwa na Yanga kutoka Lipuli FC kwani katika dakika ya 80, alipigwa kadi nyekundu na mwamuzi Hans Mabena kutokana na kumkanyaga kwa makusudi Nicolaus Wadada.

Bao la Sonso linakuwa ni la tisa msimu huu kwa wachezaji kujifunga wenyewe kwenye harakati za kuokoa.

Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi na takwimu za wachezaji waliojifunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, na mambo yalikuwa hivi...

**1. IBRAHIM SAID- (MBAO VS ALLIANCE)**

Beki wa Mbao FC Ibrahim Said alijifunga bao kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Agosti 24, mwaka jana kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Alliance. Alijifunga dakika ya 90 wakati Mbao ikiwa inaongoza bao 1-0, hivyo kuisaidia Alliance kutoka sare ya bao 1-1.

**2. GEORGE CHOTA- (MBEYA CITY VS RUVU SHOOTING)**

Ilikuwa ni Septemba 21, mwaka jana wakati beki wa Mbeya City, George Chota alipojifunga mwenyewe dakika ya 37 katika harakati za kuokoa na kuisaidia Ruvu Shooting kupata bao la kusawazisha ikicheza kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya. Tayari Mbeya City ilikuwa imeshapata bao la kuongoza dakika ya 18 likifungwa na Pater Mapunda.

**3. YASSIN MUSTAPHA- (POLISI TANZANIA VS RUVU SHOOTING)**

Ruvu Shooting ilinufaika tena na wapinzani wao kujifunga, kwani Septemba 28, mwaka jana kwenye msimu huu wa ligi, ilipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani ikicheza dhidi ya Polisi Tanzania. Alikuwa ni Yassin Mustapha wa Polisi Tanzania alipojifunga dakika ya tano tu ya mchezo na bao likabaki hilo hilo hadi mwisho.

**4. DICKSON DAUDI- (MTIBWA SUGAR VS COASTAL UNION)**

Mechi hii ilichezwa Oktoba 30, mwaka jana kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro ambapo wenyeji Mtibwa Sugar waliichapa Coastal Union mabao 2-1.

Beki wa Mtibwa, Dickson Daudi ndiye aliyeipatia Coastal bao la kufutia machozi kwa kujifunga mwenyewe dakika ya 49 katika jitihada za kutaka kuokoa.

**5. MTENJE JUMA- (COASTAL UNION VS MTIBWA SUGAR)**

Ni mechi hiyo ya Mtibwa Sugar dhidi ya Coastal Union iliyochezwa Oktoba 30, mwaka jana Uwanja wa Jamhuri ambayo imeweka rekodi ya wachezaji wawili wa timu tofauti kujifunga kwenye mechi moja.

Baada ya Dickson Daudi wa Mtibwa kujifunga, Mtenje Juma na Coastal Union ni kama alilipa, naye alijifunga dakika ya 54 na kwa bahati mbaya kwake lilikuwa ndiyo bao la pili na la ushindi kwa Mtibwa, ikiichapa Coastal Union mabao 2-1.

**6. PAUL BUKABA- (NAMUNGO VA COASTAL UNION)**

Beki wa zamani wa Simba ambaye kwa sasa anaichezea Namungo FC, Paul Bukaba, naye yumo kwenye orodha ya wachezaji waliojifunga wenyewe kwenye Ligi Kuu msimu huu hadi sasa. Alifanya hivyo Novemba 22, mwaka jana kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi.

Alijifunga dakika ya nne ya nyongeza kabla ya mechi ya Namungo dhidi ya Coastal Union kumalizika. Ilikuwa ni wakati timu yake iko nyuma kwa mabao 2-1, ikitafuta bao la kusawazisha nyumbani. Lakini wakati wakitafuta walau sare, alijifunga na kuifanya timu yake ya Namungo kupoteza mechi hiyo kwa mabao 3-1.


**7. GEOFREY LUSEKE- (ALLIANCE VS KMC)**

Geofrey Luseke, mchezaji wa Alliance alijifunga bao, kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza. Kwanza alianza kuifungia timu yake ya Alliance bao dakika ya 15, kabla ya mwenzake David Richard kufunga bao la pili dakika ya 30. Lakini kwenye dakika ya 77, Luseke alijifunga bao na kuipa KMC bao la kufutia machozi Novemba 22, mwaka jana.

**8. JUMA NYOSSO-(KAGERA SUGAR VS MTIBWA SUGAR)**

Mechi ilichezwa Novemba 26, mwaka jana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, wakati beki wa Kagera Sugar Juma Nyosso alipoingia kwenye kitabu cha mabeki waliojifunga kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Ni bao ambalo liliisaidia Mtibwa Sugar kushinda ugenini mabao 3-1.

**NAJUA WAJUA**




ARSENAL imedondosha pointi 13 ikiwa katika nafasi nzuri ya kushinda kwenye Ligi Kuu England msimu huu, idadi hiyo ikiwa ni kubwa zaidi kuliko ilivyofanya msimu mzima uliopita.

SOKA

# SABABU 'KUFELI' KWA MOURINHO SPURS



**LONDON,** England

KUMFUKUZA Mauricio Pochettino na kumleta Jose Mourinho Novemba mwaka jana linaweza kuwa moja ya kosa kubwa alilolifanya Mwenyekiti wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Daniel Levy.

**Wakati huo, alikuwa akisifiwa na kushutumiwa namna Spurs ilivyokuwa inakwenda, huku mara kwa mara akimaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu ya England na pia kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.**

Lakini akafukuzwa na saa 48 baadaye akateuliwa Mourinho kuwa kocha mpya ambaye alishakuwa kwenye viunga vya Jiji la London akiinoa Chelsea katika nyakati mbili tofauti, na pia kule Manchester United ambako alifukuzwa.

Baaada ya kuanza kwa mtazamo chanya, Tottenham kwa mara nyingine tena imejikuta kwenye wakati mgumu, ikiwa imeshinda mechi moja tu kati ya tano za mwisho kwenye Ligi Kuu na kujikuta wakiwa nafasi ya nane kwenye msimamo.

Inaonekana mambo yanakuwa magumu zaidi kwa Spurs tofauti na ilivyotarajiwa na ni wazi kwamba, Mourinho anaonekana hana uwezo wa kuidhibiti hali hiyo.

Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini kocha huyo raia wa Ureno ameshindwa kuiweka Spurs kwenye kiwango cha ubora wake.

**1. MIKATABA MIPYA KWA WACHEZAJI**

Kutokuwa na mishahara mikubwa ni moja ya sera ya Tottenham ambayo inadhibitiwa na mwenyekiti Levy pamoja na bodi yake, na imesaidia Spurs kuweza kushindana na timu kubwa licha ya kutolipa fedha nyingi. Ingawa sera hiyo imekuwa ikisapotiwa na wengi, lakini kwa soka la sasa Spurs inaonekana kuwa kwenye wakati mgumu wa kushindana na klabu nyingine kubwa za Ligi Kuu.

Wachezaji nguzo kama Christian Eriksen, Jan Vertonghen, Toby Alderweireld na Danny Rose wanaonekana kuchoshwa na maisha katika klabu hiyo ya Kaskazini mwa Jiji la London na wameshabainisha wazi kwamba wanataka kuondoka.

Ingawa Mourinho ameweza kumshawishi Alderweireld kusaini mkataba mpya, lakini morali kwenye chumba cha kubadilishia nguo si nzuri.

**2. TOFAUTI YA FALSAFA KATI YA MOURINHO NA POCHETTINO**

Hili ni jambo ambalo linaonekana linaitafuna klabu kwa namna fulani, ambalo lilitakiwa kudhibitiwa mapema tu na Tottenham. Kikosi cha sasa cha Spurs ni timu ya Pochettino – aliyoisuka yeye mwenyewe, mtazamo wa wachezaji na hata staili bado ni ile aliyoiacha kocha huyo raia wa Argentina.

Mourinho yupo kwenye kundi lenye wachezaji walio na vipaji binafsi, ambao wanaamini kwamba mafanikio ya klabu hiyo yametokana na wao. Staili mpya ya ulinzi, uchaguzi wa kikosi na mfumo mpya wa uchezaji umeondoka kabisa, utambulisho ulizoeleka wa timu hii.

Kuteuliwa kwa Joao Sacramento kutoka klabu ya Lille na kuwa msaidizi inaonyesha kwamba, Mourinho alikuwa anajua mbinu zake zinatakiwa kubadilika, lakini sasa, Tottenham inaonekana kuwa kwenye kipindi cha mpito cha falsafa mbili tofauti.

**3. KUTOKUWA NA KIKOSI KIPANA**

Wengine wanaweza kuikataa pointi hii, hasa kwa sababu Spurs ilifanya usajili wa kuwasajili wachezaji kama Giovani Lo Celso, Tanguy Ndombele na Ryan Sessegnon wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Lakini majeruhi na adhabu za kufungiwa wachezaji kumeifanya timu hiyo kukosa kikosi kipana. Na kuumia kwa hivi karibuni kwa Harry Kane, ambaye atalazimika kukaa nje kwa muda mrefu, kumezidi kukiathiri kikosi hicho kutokana na kutokuwa na wachezaji wa kutosha kwenye mzunguko wake.

Huku dirisha la usajili la kipindi cha majira ya baridi likiwa bado halijafungwa, ni wazi kwamba Levy anatakiwa kufanya jambo kwa kusajili wachezaji wa kuiongezea nguvu timu hiyo.

TANGU kuanza kwa mwaka 2019, ni Liverpool (19), Man City (17) na Spurs (12) pekee zilizoshinda mechi nyingi za Ligi Kuu za nyumbani zaidi ya Newcastle (11).

PREMIER LEAGUE

NDANI YA 18

Nipashe Spotika



MICHUANO ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya timu 16-bora, ratiba yake imepangwa kufanyika Februari 2020. Timu sita zilifuzu kwa hatua hiyo msimu huu kwa...

Uk. 16&17

# REKODI 3 ZA RONALDO ZINAZOMTESA MESSI



RONALDO

**TURIN,** Italia

LIONEL Messi, pamoja na Cristiano Ronaldo, wamekuwa kwenye kiwango cha juu zaidi kwa kipindi cha muongo mmoja kuanzia mwaka 2010 hadi 2019.

Wafungaji walioweka rekodi ya wakati wote kwa Barcelona na Real Madrid, Messi na Ronaldo ndio wachezaji pekee waliofunga mabao 300 au zaidi kwenye Ligi Kuu ya Hispania na mabao 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji hao wawili wote wameweka rekodi ya kufunga 'hat-trick' kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Messi anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ronaldo anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi hatua ya mtoano.

Kiwango cha Messi na Ronaldo kinawafanya kuwa wachezaji pekee waliofunga hat-trick 50 au zaidi kwa klabu zao na nchi. Wote wawili wana 'hat-trick' nyingi zaidi kwenye LaLiga, Messi akiwa na 35, huku Ronaldo akiwa na 34.

Makala haya yanaangalia rekodi tatu za Ronaldo ambazo zinaweza zisifikiwe kabisa na Messi hadi anastaafu kucheza soka, zifahamu...

**1. KUFUNGA KWENYE FAINALI LIGI YA MABINGWA ULAYA NA TIMU MBILI TOFAUTI**

Mmoja wa kundi la wachezaji ambao wameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nyingi zaidi ni Cristiano Ronaldo. Lakini yeye ni mchezaji pekee kuwahi kufunga kwenye fainali na timu mbili zofauti ambazo zilitwaa ubingwa huo.

Raia huyo wa Ureno aliifungia Manchester United kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea msimu wa 2007-08 na pia alifunga kwenye fainali akiwa Real Madrid dhidi ya Atletico Madrid msimu wa 2013-14 na fainali dhidi ya Juventus msimu wa 2016-17.

Messi ameifungia Barcelona kwenye fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya, msimu wa 2008-09 na ule wa 2010-11 - zote ni kati ya Barcelona dhidi ya klabu ya Ligi Kuu ya England Manchester United.

Huku Messi akionekana kutokuwa na mpango wa kuondoka hapo Barcelona, rekodi hii inaonekana itaendelea kushikiliwa na Ronaldo dhidi ya Messi.

**2. KUSHINDA TAJI LA LIGI KUU TATU**

Ronaldo ni mchezaji pekee ambaye ameshinda mataji katika ligi tatu kubwa kati ya tano za Ulaya - England (Manchester United-3), Spain (Real Madrid-2) na Italia (Juventus-1).

Messi ameshinda mara saba taji la Ligi Kuu ya Hispania akiwa na Barcelona pekee.

Na kwa kuwa inaonekana ni ngumu kwa Messi kuondoka Barcelona hataweza kuifikia rekodi hii ya Ronaldo.

**3. MATAJI MENGI KIMATAIFA**

Mchezaji pekee kufunga kwenye michuano minne tofauti ya Mataifa ya Ulaya (Euro 2004, 2008, 2012, 2016), Cristiano Ronaldo alimaliza ukame wa miaka 12 wa kupata taji kwenye timu ya taifa wakati alipobeba lile la Euro 2016 akiwa na Ureno baada ya kuifunga bao 1-0 Ufaransa.

Ronaldo alipoteza fainali yake ya kwanza kwenye Euro 2004 wakati Ureno ilipofungwa na Ugiriki. Tangu hapo, Ronaldo pia ameshinda taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa akiwa na Ureno.

Messi, kwa upande mwingine bado hajawahi kushinda taji la kimataifa akiwa na Argentina, akishindwa kwenye fainali tatu kubwa - Kombe la Dunia mwaka 2014 dhidi ya Ujerumani na fainali mbili za Copa America mwaka 2015 na 2016 dhidi ya Chile. Ni wazi kwamba, Messi anaweza kumaliza kipindi chake cha uchezaji bila ya kuzifikia rekodi hizo za Ronaldo.

**USILOLIJUA**

KATIKA timu zinazoshiriki Ligi Kuu England, Arsenal ndiyo imetoka sare nyingi (11) msimu huu kuliko timu zingine, ukilinganisha na msimu mzima uliopita ambao ilimaliza na sare 12 tu.





Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Prof. Elifas Bisanda (kushoto), akizungumza na viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo hicho (OUT) katika Tawi la Mbeya mwishoni mwa wiki. Kulia ni baadhi ya viongozi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wafanyakazi 200 wagoma kudai mishahara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya wafanyakazi 200 wa Kampuni ya China Railway Seventh Group (CRSG) ambayo inajenga barabara ya Iyunga Viwandani yenye urefu wa kilometa sita na mtaro wa maji katika eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani jijini Mbeya, wamegoma kufanya kazi wakishinikiza walipwe mishahara yao ya miezi mitatu huku wakifanya fujo.

Wafanyakazi hao walizua kizazaa hicho juzi kwa kukusanyika mbele ya lango kuu la ofisi za kampuni hiyo zilizopo eneo la Iwambi wakiwa wamebeba mabango yenye jumbe mbalimbali, huku wakiimba nyimbo za hamasa za kudai walipwe mshahara wao.

Hali hiyo ilisababisha viongozi wa juu wa kampuni hiyo kukimbilia kwenye magari na kuondoka haraka eneo la ofisi hizo na kuwaacha wafanyakazi hao wakiendelea kuimba nyimbo zao wakiwa wamebeba mabango.

Wakizungumza na waandishi wa habari, baadhi ya wafanyakazi hao walisema wameamua kugoma baada ya kuona viongozi wa kampuni hiyo hawawajali kwa kutowalipa mishahara yao kwa miezi mitatu mfululizo liche ya kufanya kazi kwa uadilifu.

Mhandisi Richard Mbilinyi, alisema hawajalipwa mishahara yao tangu Novemba mwaka jana, hali ambayo imesababisha maisha yao kuwa magumu huku wakikabiliwa na majukumu ya kuhudumia familia zao.

"Tumesherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa shida bila kuwa na fedha na sasa tunakabiliwa na majukumu ya kupeleka watoto shuleni, lakini hatuna fedha, hali imekuwa ngumu kiasi kwamba tunashindwa hata kupata chakula," alisema Mbilinyi.

Alisema wameshachukua hatua mbalimbali za kudai haki zao kistaarabu, ikiwa ni pamoja na kwenda kuwaona viongozi wa serikali mkoani Mbeya ili wawasaidie walipwe fedha zao, lakini jitihada zao zimegonga mwamba.

Alisema walimuona Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Jiji, lakini wote wameshindwa kuwasaidia na kwamba walijaribu kumtafuta Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila ili awasaidie lakini kila wakienda ofisini kwake walikuwa wanamkosa.

Naye Agosti Simon, alisema tangu waajiriwe na kampuni hiyo hawajawahi kulipwa mishahara yao kwa wakati na ucheleweshaji huo wa mishahara umekuwa ukiongezeka kila mwezi na sasa imefikia hatua wanakaa mpaka miezi mitatu bila kulipwa.

"Tangu tuajiriwe hapa tunaishi kwa taabu tu, hakuna mwezi ambao wanatulipa mshahara kwa wakati, kila mwezi unapomalizika wanasema hakuna fedha wanatulipa kuanzia tarehe kumi ya mwezi unaofuata na sasa wametuacha mpaka imemalizika miezi mitatu bila kulipwa, kwa kweli inatuumiza sana tunaomba msaada," alisema Simon.

Alisema hali hiyo haiwezi kuvumilika kwa vile inaathiri maisha yao, hivyo wanaiomba Serikali Kuu iingilie kati kuhakikisha wanalipwa fedha zao.

Viongozi wa kampuni hiyo baada ya kuona waandishi wa habari wakifika eneo la ofisi hizo waliamua kupanda magari na kuondoka bila kuzungumza chochote, huku baadhi yao wakizongwa na wafanyakazi kuwazuia wasiondoke, hali ambayo ilisababisha tafrani katika eneo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, hakupatikana kuzungumzia mgogoro huo kwani baada ya waandishi kufika ofisini kwake walielezwa kuwa alikuwa amekwenda wilayani Mbarali kwa ziara ya kikazi na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi ya Mkoa.

# Serikali yaombwa walimu wa kike

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Ilota iliyopo Kata ya Mshewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Joel Munuo, ameiomba serikali kuwapatia mwalimu wa kike shuleni hapo ili kukabiliana na matatizo yanayowakumba watoto wa kike wanapokuwa hedhi.

Munuo alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na Nipashe, alisema tangu kuanzishwa kwa shule hiyo mwaka 1991 hawajawahi kupata mwalimu wa kike jambo ambalo limechangia utoro kwa mabinti wanapokuwa hedhi.

Alisema mara kwa mara wamekuwa wakiikumbusha halmashauri kuwapatia mwalimu wa kike, lakini wanapewa jibu la kuwa wasubirie wako kwenye mchakato.

Alisema shule hiyo ina walimu watano na wanafunzi 250, hivyo hitaji lao ni kupata walimu wawili wa kike ili kukidhi mahitaji kwa mabinti.

"Tunaomba wadau wengine wa kulisema hili suala la kukosekana kwa mwalimu wa kike shuleni hapa mimi pamoja na wenzangu tumejitahidi kuikumbusha serikali kutuletea mwalimu lakini hadi sasa hakuna, wanaume hatuwezi kuwahudumia vyema mabinti wanapokuwa kwenye siku zao ukilinganisha na wanawake, tunalazimika kufanya jukumu hilo kwa sababu hakuna namna," alisema Mwalimu Munuo.

Aliongeza kuwa wanashindwa kuwahudumia watoto wanaokuwa wa hedhi ipasavyo kwa sababu hawana uhuru wa kuwaeleza masuala mbalimbali ya hedhi salama na namna ya kujisitiri kama ambavyo kungekuwapo na walimu wa kike.

Alidai kazi kubwa wanayoifanya ni kuwapa uhuru watoto wote wa kike ambao wanafikia umri wa kubalehe na kupata hedhi kutoa taarifa pindi wanapoona mabadiliko kwenye miili yao ili wawasaidie.

Alisema licha ya kujitahidi kuwa karibu na watoto hao, lakini tatizo lilipo ni ukosefu wa chumba maalum cha watoto kujisitiri pamoja na taulo za kike na kwamba wakati mwingine hulazimika kutumia fedha zao kuwanunulia pedi.

Mtendaji wa Kijiji cha Ilota, Daud Livingstone, alisema kukosekana kwa mwalimu wa kike shuleni hapo kumesababisha baadhi ya wazazi kuwahamisha mabinti zao shule wakihofia kukosa elimu ya hedhi salama.

Alisema wakati mwingine wazazi au walezi hulazimika kwenda shuleni kuwahudumia watoto wanaokuwa hedhi.

Diwani wa Kata ya Mshewe, Esther Mbega, alisema tatizo la kukosekana kwa mwalimu wa kike, shule ya msingi Ilota alilikuta tangu anaingia madarakani mwaka 2015 na kwamba anajitahidi kuwasilisha suala hilo kwenye vikao vya madiwani.

# Wana-Kyela wajitosa sekta za elimu, afya

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAKAZI wa Wilaya ya Kyela waishio maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi, wanaounganishwa na mtandao wa kijamii wa Whatsapp kupitia kikundi cha Kyela Social Economic (Kyeseg), wameahidi kuboresha sekta ya afya, elimu na kuwasaidia wenye uhitaji ikiwa ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii yao.

Akizungumza na Nipashe jana Mwenyekiti wa kikundi hicho, Shadrack Mwamakula, alisema kikundi hicho kilianzishwa tangu mwaka 2014 kikiwa na lengo la kuwaunganisha wana-Kyela kwenye maeneo wanayoishi, lakini kutokana matatizo yaliyoko kwenye sekta za afya na elimu walikubaliana kila mwisho wa mwaka wanakutana Kyela kujadili na kutatua vikwazo kwenye sekta hizo.

Alisema sekta ya afya inakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo uchakavu wa majengo, uhaba wa vifaa tiba, suala la elimu ni ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia hasa kwenye masomo ya sayansi, mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi pamoja na walimu.

Katika kutatua masuala hayo mwaka jana walinunua vifaa tiba vya kujifungulia kwenye wadi ya wazazi vyenye thamani ya Sh. milioni mbili ambavyo vilikabidhiwa Hospitali ya Wilaya ya Kyela.

"Awali kikundi chetu kilitukutanisha kwa lengo la kula na kunywa kwenye maeneo tunayoishi, mawazo yalitolewa juu ya kuisaidia jamii yetu ya Kyela kwenye nyanja ya afya na elimu na tulikubaliana tukaanza kuchangishana fedha, tufanikiwa kununua vifaa tiba vya kujifungulia na kukabidhi hospitali ya wilaya na kufanya usafi, pamoja na matukio mengine ikiwamo ngoma za jadi," alisema Mwamakula.



# TBS yateketeza vyakula, vipodozi feki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeteketeza bidhaa za vyakula na vipodozi ambazo havikidhi viwango katika soko zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkuu wa Kanda ya Kati, Salome Emmanuel, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye uteketezaji wa bidhaa hizo jijini hapa.

Alisema bidhaa hizo zimekamatwa katika mikoa ya Dodoma na Singida, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2019.

"Bidhaa hizi nyingi ni za vyakula pamoja na vipodozi nyingi zimekamatwa kwa wafanyabiashara wa rejareja ambapo nyingi zimebainika kukosa ubora katika soko kwa kuisha muda wa matumizi, lakini zikiendelea kuuzwa katika maeneo mbalimbali," alisema. Aliwataka wafanyabiashara ambao wamekuwa na tabia hiyo ya kuuza bidhaa ambazo zimeisha muda wake kuacha mara moja kwani atakayebainika sheria itachukua mkondo wake.

"Pia nitoe wito kwa wananchi kuwa makini wakati wananunua bidhaa mbalimbali za vyakula pamoja na vipodozi ili kuepuka kutumia bidhaa ambazo hazikidhi ubora katika soko na kuepukana madhara yanayoweza kuwapata ya kiafya," alisema.

Alisema kuwa ukaguzi wa bidhaa katika maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo utakuwa endelevu ili kuhakikisha kuwa katika soko hakuna bidhaa zisizokidhi viwango.

Naye, Mkazi wa Jiji la Dodoma, Halima Saidi, alisema kuwa shirika hilo linatakiwa kuongeza nguvu katika ukaguzi wa bidhaa kutokana na wafanya biashara kubuni mbinu mbalimbali za kufanya uhalifu huo.

Alisema hivi sasa kumekuwa na wimbi la bidhaa bandia katika masoko mbalimbali.

"Tunaomba zoezi hili kuwa endelevu kwani hawa wafanyabiashara siku hizi wamekuwa na mbinu za hali ya juu sana katika kughushi hadi muda wa matumizi wa bidhaa hasa zile za vyakula na kibaya zaidi maziwa ya watoto wachanga ambao wanatakiwa kupata vitu vyenye ubora," alieleza Saidi.



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Mkoa wa Dodoma, wakiendelea kuwahudumia wananchi, kutokana na idadi kubwa kuendelea kujitokeza kupata vitambulisho kabla ya kufungwa kwa zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya vidole leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hasunga ampa kibarua kizito mrajis wa ushirika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amemwagiza Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na Watendaji wa Tume ili kufanya mabadiliko yatakayoongeza ufanisi.

Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na Viongozi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini.

Hasunga alisema kuwa kero nyingi zinazojitokeza katika sekta ya ushirika zinasababishwa na baadhi ya warajis wasaidizi kutokusimamia ipasavyo vyama vya ushirika vilivyopo katika maeneo yao.

"Mrajis, fanya tathmini ya warajis wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na watendaji wa tume kwa ujumla na ikiwezekana fanya mabadiliko muhimu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa vyama vya ushirika," alisema Hasunga aliagiza watumishi wa Tume waliopo makao makuu wapunguzwe na kuhamishiwa kwenye ofisi za tume katika ngazi za mikoa na wilaya ili kuongeza nguvu ya usimamizi wa vyama hivyo ngazi ya mikoa na wilaya.

Kufuatia maelekezo ya Waziri Hasunga, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege, aliahidi kutekeleza malekezo yaliyotolewa ili kuimarisha utendaji kazi wa Tume kwenye usimamizi wa vyama vya ushirika nchini.

Alisema yote waliyoagizwa watayafanya ipasavyo ili kuhakikisha wanaboresha utendaji wa kazi zao.

Alieleza lengo lao ni kuona vyama vya ushirika vinakuwa imara na kusaidia wakulima katika maeneo mbalimbali nchini.

# Mrundikano wa taka dampo wamkera Jafo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, amekerwa na mrundikano wa taka kwenye madampo ya kisasa yaliyojengwa kwenye baadhi ya majiji na manispaa na kuagiza mitambo ya kuchakata itumike kwa asilimia 100.

Madampo hayo yalijengwa kupitia mradi wa uendelezaji miji ya kimkakati Tanzania (TSCP).

Hali hiyo ilijitokeza jana katika ziara yake Jafo ya kutembelea dampo la kisasa Jiji la Dodoma lililojengwa Chidaya na kubaini baadhi ya vifaa kutofanya kazi na kusababisha kazi ya usambazaji na ukandamizaji wa taka kufanyika taratibu.

Alisema madampo hayo yamejengwa kwa gharama kubwa ili kuimarisha usafi na kuchakata taka hizo kwa utaalamu wa kisasa ambao hausababishi athari za kimazingira.

"Inashangaza kuona mitambo ya kuchakata taka imeegeshwa tu haifanyi kazi na takataka zimerundikana hapa, sioni sababu ya uongozi wa dampo kushindwa kushindilia hizi taka kila zinapoletwa, matokeo yake mnasababisha inzi na harufu kwenye dampo," alisema.

Jafo aliongeza kuwa "Nilipotembelea Kigoma nilikuta mitambo pia imeegeshwa tu bila kufanya kazi inayotakiwa na niliwaambia kuwa nitahamisha mitambo ya Kigoma kuleta Dodoma, kwa hali hii siwezi kuleta ile mitambo rekebisheni yenu haraka."

Waziri huyo alitoa wiki mbili kwa uongozi wa Jiji la Dodoma, kuhakikisha vifaa vinavyotumika kwenye dampo la Chidaya vinafanya kazi kwa asilimia 100 na kuongeza usimamizi wake ili kuimarisha usafi Makao Makuu ya Nchi.

"Hali niliyoikuta katika dampo hili inaonesha kuwa kuna mahali watendaji wa halmashauri hawawajibiki ipasavyo," alisema.

Awali, Ofisa Mwendeshaji wa dampo hilo, Peter Madono, alisema mvua zimekuwa zikichelewesha utendaji kazi kutokana na mitambo hiyo kushindwa kufika kwenye dampo hilo.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema halmashauri imetenga bajeti ya Sh. milioni 600 kwa ajili ya matengenezo ya vifaa hivyo vinapopata hitilafu.

Jafo alilazimika kufunga safari hadi karakana ya jiji, ili kuangalia mtambo unaodaiwa kuharibika Desemba mwaka jana, ambao unaendeshwa na Ester Nyenge na kuangizwa kutengenezwa haraka huku akitaka mkurugenzi kumwongezea mshahara.





# Majaliwa aonya maofisa kilimo wanaokaa ofisini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri na Mabaraza ya Manispaa Zanzibar, kuwatoa maofisa kilimo na uvuvi wanaokaa maofisini badala ya kwenda vijijini kushughulikia kero za wakulima na wafugaji.

Aliwataka maofisa hao kufanya kazi kwa vitendo na kuacha kukaa ndani maofisini wakati wakulima na wavuvi wanachangamoto nyingi zinazowakabili zinahitaji kutatuliwa.

Akizungumza juzi baada ya kukagua kilimo cha kisasa huko Jozani Mkoa wa Kusini Unguja, alisema kuwa wakulima wanahitaji taaluma ili kuweza kuendeleza kilimo hivyo ni vyema maofisa wa kilimo kwenda mashambani kwa wakulima kutoka taaluma hiyo. "Waondoeni wale wote maofisa kilimo wanaokaa maofini wapelekeni vijijini na ikiwezekana wajengeeni nyumba wawe wanaishi huko huko hakuna kukaa mjini," alisema Majaliwa.

Aidha, aliwapongeza wananchi wa Kijiji cha Jozani kwa kuanzisha ushirika wa kilimo cha kisasa, ambapo kilimo cha ushirika kinasaidia kupata mafanikio ya haraka kuliko kilimo cha mtu mmoja.

Katika hatua nyingine Waziri Mkuu alikagua kituo cha ubunifu wa kisayansi (School hubs) cha Bwejuu Mkoa wa Kusini Unguja, ambapo aliwaagiza makandarasi wanaojenga kituo hicho kukamilisha kazi hiyo baada ya mradi huo kuchelewa kukamilika kwa muda uliopangwa.

Alisema mradi huo ulipangwa kukamilika Desemba mwaka jana, lakini hadi sasa bado haujakamilika hivyo aliwaagiza makandarasi hao kukamilisha ujenzi huo ambao unakusudia kuimarisha masomo ya sayansi kwa wanafunzi. "Haya ni maamuzi ya serikali kujenga vituo hivi ili kuongeza ufaulu katika masomo ya sayansi," alisema Waziri Mkuu huyo.

Alisema ili nchi iweze kuzalisha wanasayansi wengi ni lazima kuweka mkakati madhubuti katika masomo ya Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hesabu ili kufikia malengo ya nchi ya uchumi wa kati kupitia viwanda.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema lengo la ujenzi wa vituo hivyo ni kuhakikisha wanaondosha tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi na kuwa na wataalamu wengi hapo baadaye.




Mfanyabiashara Visiwani Zanzibar, Salum Turkey, akitoa maelezo kwa waandishi wa habari kuhusu boti yake mpya ya abiria itwayo Zanzibar One ambayo imeanza safari yake juzi kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ...Asifu wanawake kujitokeza kupima VVU kuliko wanaume

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuwa amebaini kuwa wanawake ndiyo wanajitokeza kupima virusi vya ukimwi kuliko wanaume.

Aidha, alisema kiwango kikubwa cha wanaume ni waoga kupima VVU na badala yake wamekuwa na tabia ya kufurahia matokeo ya wake zao pale wanapogundulika kuwa hawana maambukizi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa kituo kipya cha afya ya mama na mtoto katika eneo la Bambi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alieleza kuwa malengo ya Serikali ya Tanzania na Zanzibar kwa mwaka huu kila Mtanzania kupima afya yake na kujijua kama hana maambukizi ya virusi vya ukimwi.

"Tunataka kila mmoja kupima ukimwi na kujitambua usiwe na woga...kwenye malengo haya tumeondoa kipengele cha woga tunataka watakaotambulika kuwa na virusi vya ukimwi waweze kutumia dawa za kufubaza virusi," alisema.

Alisema kuwa wanaume ndio wanaochelewesha malengo ya serikali ya kufikia asilimia 90 katika upimaji wa VVU kwa wananchi wake.

"Wanaume mmekuwa na tabia ya kufurahia matokeo ya wake zenu iwapo wakigundulika hawana ukimwi, msijidanganye wanaume hayo majibu ni ya wake zenu nendeni mkapime na nyinyi msitegemee majibu ya wake zenu," alisema Majaliwa.

Pia aliwataka kinamama kuwahimiza waume zao kupima hata wakigundulika kuwa na VVU wasitoke katika ndoa na badala yake kuwahimiza watumie dawa za kufubaza na kufuata utaratibu wa kukaa na waume zao.

Majaliwa alisema serikali imeweka msisitizo katika sekta ya afya msisitizo wa huduma ya mama na mtoto na vifo vya mama na mtoto vimepungua baada ya kuimarisha huduma hizo.

Alisema hakuna haja sasa kwa kinamama kujifungulia nyumbani na kuhakikisha wanajifungulia hospitalini ili kuweza kunusuru afya zao na mtoto. Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Hamida Mussa, aliwataka kinamama wajawazito kuhudhuria kliniki kwa wakati ili kuweza kuondokana na matatizo wakati wa kujifungua.

"Hivi sasa huduma za afya ya mama na mtoto zipo karibu hapa kijijini penu hakuna sababu tena ya kutohudhuria kliniki au kujifungulia nyumbani," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

# Wawekezaji wasisitizwa kufuata sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAWEKEZAJI wametakiwa kuzingatia sheria za nchi, na kutimiza wajibu wao katika kuleta maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla.

Akifungua mkutano wa wawekezaji wa sekta mbalimbali za mkoa wa Kusini Unguja juzi katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza), Mkuu wa mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kufanya hivyo kutachochea kasi ya maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Alisema wawekezaji wamekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na kuimarisha ujuzi kutokana na shughuli wanazoziendesha, hivyo nia ya mkoa wake ni kuwafanya wawe imara zaidi ili waongeze mchango wao katika uchumi.

"Lengo la kukutana hapa ni kuona ni kwa namna gani tunaweza kuendeleza dhana ya uwekezaji kwa manufaa ya pande zote, serikali, jamii na nyinyi kwani mmekuwa na mchango muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na watu wake," alieleza Ayoub.

Aidha, aliwaomba wawekezaji hao kuzitumia ofisi za wakuu wa wilaya na taasisi nyingine za serikali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zinazohusu shughuli zao hususani suala la umiliki wa ardhi.

"Katika suala la ardhi niwaombe msiwatumie watu wa katikati au madalali kwani tumegundua kuwa ndio chanzo cha migogoro mingi ya ardhi katika baadhi ya maeneo ya mkoa wetu. Ni vyema mkazitumia ofisi zetu, lakini taasisi zinazohusiana na ardhi kupata huduma ili kuepukana na migogoro isiyo ya lazima," alisema.

Kuhusu suala la usalama ambalo lilielezwa na wawekezaji hao ni moja ya changamoto inayowakabili, alieleza kuwa ipo haja ya kuwa na mpango wa pamoja wa ushirikiano utakaoongeza hali ya usalama kwa wageni na wenyeji wanaotumia huduma zinazotolewa na wawekezaji hao.

"Katika mkoa wetu kuna hoteli za kitalii na taasisi nyingine zinazotoa huduma kwa wageni zaidi ya 200. Hii ni nguvu kubwa tunayoweza kuitumia kustawisha ulinzi na usalama siyo kwa kuongeza vituo vya polisi tuu bali pia kuweka mifumo ya ulinzi," alisema.

Aidha, aliwapongeza wawekezaji hao kwa kuamua kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na kuwaomba kuendelea kushirikiana na wenyeji ili dhana ya uwajibikaji kwa jamii iwe na tija kwa jamii badala ya watu wachache.

Kwa upande wao wawekezaji hao walisema pamoja na mafanikio waliyonayo bado wanakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo za usalama, uchafu wa mazingira hasa ya fukwe na vitisho vya baadhi ya watendaji wa sekta za serikali wanaokwenda kupata taarifa za maendeleo au shughuli zao.

Walieleza kuwa kuna baadhi ya watendaji wa taasisi za serikali wanapokwenda katika maeneo yao hawatumii lugha nzuri au kufuata taratibu jambo ambalo linapelekea mikwaruzano baina yao na wakuu wa hoteli.

# Tanapa yaipiga jeki Ikungi mil. 24/- madawati shule

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida Sh. milioni 24 kwa ajili ya kutengeneza seti za viti na meza 400, ili kukabiliana na upungufu wa madawati kwenye shule za sekondari wilayani humo.

Akitoa taarifa ya ugawaji wa madawati 330 katika shule saba kati ya 30 za sekondari zilizopo. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema kuna jumla ya wanafunzi 4,517 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wilayani humo.

Alisema kwa mwaka huu Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imeongeza ufaulu kutoka kwa wanafunzi 1,483 waliokuwapo mwaka 2018 hadi kufikia wanafunzi 4,787 mwaka huu ikiwa ni sawa na asilimia 83.63 na hivyo kuwawezesha kushika nafasi ya kwanza kwa Halmashauri za Mkoa wa Singida.

"Nitatoa takwimu chache kwamba mwaka 2019 kidato cha nne waliofaulu daraja la kwanza ni takribani wanafunzi 103, daraja la pili 218, daraja la tatu ni 329 na daraja la nne ni 1,037," alifafanua Kijazi.

"Ukilinganisha na mwaka 2018 ufaulu ulikuwa daraja la kwanza wanafunzi 53, daraja la pili 182, daraja la tatu 279 na daraja la nne 969, ongezeko kubwa kwa mwaka huu ambapo tumeweza kufaulisha kwa takribani asilimia 83.63 na kuwa wa kwanza kimkoa," alifafanua.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kutokana na uhaba wa madawati, ongezeko la katika shule za sekondari za halmashauri na ufaulu, lakini hakuna mwanafunzi hata mmoja ambaye hataweza kuingia darasani kwa sababu wana vyumba vya madarasa vya kutosha na wanatengeneza madawati na kukarabati yaliyovunjika.

Alisema halmashauri hiyo inahitaji viti na meza 13,076 ili kukidhi mahitaji ya shule 30 na hadi sasa halmashauri ina viti 9,557 na meza 9,509 kwa shule zote za umma.

Kijazi alibainisha kuwa walitakiwa kutengeneza viti na meza 1,670 ili kuweza kukidhi ongezeko kubwa la wanafunzi ambao wanaingia kidato cha kwanza na kwamba mpaka sasa wametengeneza na mezi 330 na kukarabati meza na viti zaidi ya 800.

Akikabidhi madawati hayo kwa shule saba za sekondari, Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogoro, alisema kuwa jitihada mbalimbali zinafanyika kuboresha elimu wilayani humo na ndiyo maana imekuwa wilaya iliyofanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha nne.

Aidha, alisema katika kuimarisha elimu ya ufundi wamepokea Sh. bilioni 4 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama pamoja na Chuo cha Ufundi Stadi (Veta).

Naye Ofisa Elimu Sekondari, Ngwano Ngwano, alisema halmashauri hiyo iliomba kiasi cha Sh. milioni 24 kutoka Tanapa na wanatarajia kutengeneza madawati zaidi ya 588.




Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogoro (kushoto), akimkabidhi mmoja wa walimu wa shule za sekondari za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi madawati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wavuvi wapata neema ya soko

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WAVUVI wilayani Kalambo mkoani Rukwa, wamepata soko la uhakika la kuuzia samaki baada ya halmashauri hiyo kuwaruhusu kuuza kwa kutumia soko la kutoweo hicho la kimataifa.

Soko hilo lilijengwa katika kijiji cha Kasanga mwambao wa Ziwa Tanganyika wilayani humo.

Soko hilo lililopo Kasanga ni moja kati ya masoko mawili ya kimataifa yaliyopo wilayani Kalambo, ambapo soko jingine ni la mazao lililopo katika mji wa Matai, yaliyojengwa kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka 2011 kupitia mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania (Mviwata).

Ujenzi wake ulifadhiliwa kwa asilimia 80 na Jumuiya ya Ulaya (EU), huku Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, kabla ya kugawanywa na kuanzishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, ikichangia asilimia 20 ya ujenzi huo.

Lengo la mradi huo, ni kuwaunganisha wakulima ili wawe na sauti moja katika kushawishi na kutetea maslahi yao kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Soko la kimataifa la kuuzia samaki liko umbali wa kilomita 73 kutoka mji wa Matai ambao ndio makao makuu ya wilaya likilenga kuwanufaisha watu 35,205 wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika na watu 238,000 kutoka maeneo mengine ya Wilaya ya Kalambo sambamba na mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma pamoja na nchi jirani za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Rwanda na Burundi.

Soko hilo ni fursa kwa wavuvi watakao kuwa wanauza samaki na mazao yake yatakayo kuwa yakivuliwa katika Ziwa Tanganyika na kuuzwa maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kupitia soko la samaki la Kasanga.

Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, imewataka wafanyabiashara wote wa samaki wa ndani na nje ya nchi kufika kwa wingi katika soko la samaki la Kasanga ili wapate samaki kwa wingi na wenye ubora wa kiwango cha kimataifa kwa ajili ya kukuza mitaji yao na maendeleo ya Kalambo na taifa kwa ujumla.

Samaki wanaopatikana kwenye eneo hilo ni aina ya sangara, kuhe, migebuka, samaki wa mapambo, dagaa wakubwa na aina nyingine nyingi za samaki.

Mmoja wa wavuvi waliopo katika Kijiji cha Kasanga mwambao wa Ziwa Tanganyika, Skeva Sinyangwe, aliishukuru serikali kwa kuruhusu soko hilo kuanza kutumika kwani litawaondolea changamoto walizokuwa wakikutana nazo hapo awali ambapo walikuwa wakitegemea kuuza samaki wao kwa kutumia masoko yaliyopo nchi jirani.

# Wanawake wapewa msukumo kugombea uongozi mwaka huu

INATOKA UK. 9

yake ya wanaume wa kuleta mabadiliko kwa kujitolea kwa kuwafikia wanawake mpaka vijijini, jambo ambalo litasaidia kuwazindua na kujua kwamba ni haki yao kuwa viongozi.

Alisema, katika Wilaya ya Mkoani kuna madiwani 13, kumi (10) ni wanaume na wa tatu ni wanawake kati ya madiwani hao... sasa tunataka mwaka 2020 tuwaone wanaingia majimboni kugombea ili wawe wengi," alisema.

Naye Diwani wa Mkoani, Mohamed Said Ali, alieleza kuna umuhimu mkubwa kwa wanawake kupatiwa elimu itakayowashawishi kuondokana na dhana potofu walizonazo juu ya kuongoza, ili waweze kuingia kwa wingi kwenye mchakato wa kugombea nafasi hizo kwa maendeleo endelevu ndani ya nchi.

Alisema kuwa, endapo mwanamke ataweza kujielewa mapema juu ya umuhimu wa kugombea nafasi hizo basi kuna uwezekano wa kutetea wenzake walio katika hali duni na kuwaletea maendeleo endelevu, jambo ambalo ndio azma ya serikali.

Aidha, aliwataka wanawake kutosahau mila na desturi na maadili ya dini yao hasa katika suala zima la kuheshimu ndoa zao, familia zao katika kipindi cha kwenye uongozi wao, ili kuepukana na changamoto zinazojitokeza.

Hidaya Omar Hamad mkaazi wa Mjimbini alieleza kuwa, bado wanawake wengi wana dhana ya kuwa wakimchagua mwanamke mwenzao atawaletea maringo na hata kuwazarau.

"Ni vizuri wanawake wenzangu tukaondokana na dhana hiyo, tugombee nafasi za uongozi majimboni na tuwape kura ambao watajitokeza kugombea," alisema mwananchi huyo.

Naye mwanannchi ambae hakutaka jina lake litajwe aliwataka wanawake wenzake kuachana na tabia ya kufikiriana vibaya na uchoyo katika nafsi zao, badala yake wawachague ili ifikapo mwaka 2020 waingie kwa wingi katika vyombo vya kutoa maamuzi, jambo ambalo litasaidia kuleta maendeleo katika nchi.

Tamwa kisiwani Pemba imeunda timu maalumu ya wanaume 10 wa kuleta mabadiliko katika jamii, juu ya umuhimu wa wanawake kugombea nafasi za uongozi.

## Isabel dos Santos kuwania kiti cha urais Angola

**LUANDA,** Angola

BINTI wa Rais wa zamani wa Angola, Dos Santos, Isabel dos Santos, amesema anafikiria kuwania urais mwaka 2022.

Isabel (pichani chini), kama wengi wa wanafamilia ya Dos Santos, aliondoka Angola, akidai alikabiliwa na vitisho vya kuuliwa baada ya baba yake kuondoka madarakani.

Isabel anayeaminiwa kuwa mwanamke tajiri zaidi barani Afrika anachunguzwa kwa madai ya kufanya ubadhirifu wa fedha na kuzisababishia hasara kubwa kampuni za serikali ikiwa ni pamoja na kampuni kubwa ya mafuta ya taifa Sonangol.

Viongozi wa mashtaka nchini Angola walizuia mali zake anazomiliki na mume wake Sindika Dokolo, raia wa DRC.

Taarifa zaidi zinasema kuwa hisa zao katika kampuni kadhaa za Angola, pamoja na kampuni ya simu ya Unitel na kampuni ya simenti ya Cimangola, pia zimeshikiliwa na mahakama.

Mwanzoni mwa mwezi huu Isabel alisema madai hayo dhidi yake yamechochewa kisiasa.

Isabela aliteuliwa kuwa mkuu wa kampuni ya matuta ya taifa Sonangol mnamo mwaka 2016, lakini alitolewa kwenye wadhifa huo mwaka uliofuata katika hatua ya kwanza iliyofanywa na Rais wa Angola, Joao Lourenco ya kuwaondoa jamaa za Dos Santos kutoka kwenye nyadhifa mbalimbali.

Baba yake Jose Eduardo dos Santos aliitawala Angola kwa miaka 38 na utawala wake unahusishwa na kukithiri kwa ufisadi na ubaguzi. **RFI**



# Mawakili wafunguka tuhuma zinazomkabili Rais Trump

**WASHINGTON,** Marekani

JOPO la mawakili wa Rais wa Marekani, Donald Trump kwa mara ya kwanza limetoa majibu rasmi kuhusiana na mashtaka yanayomkabili mteja wao likisema kuwa ni vita vikali dhidi ya demokrasia.

Taarifa ya mawakili hao ilieleza kuwa vifungu vya sheria kuhusu hoja ya kumwondoa Rais Trump madarakani havikutaja makosa yoyote yaliyofanywa na kuongeza kuwa ni njama ya jaribio la kuingilia uchaguzi wa urais wa mwaka 2020.

Kauli hiyo wameitoa wakati wajumbe wa chama cha Democrats wamewasilisha malalamiko yao kabla ya kuanza wa kesi hiyo wiki ijayo.

Rais Trump anakuwa ni rais wa tatu wa Marekani kukabili na mashtaka kama hayo.

Rais Trump anatuhumiwa kwa kutumia vibaya mamlaka yake na kuzuia Bunge la Congress kufanya uchunguzi.

Hata hivyo, amepinga kufanya kosa lolote na kutaja kesi dhidi yake kuwa ya uongo.

**Rais Trump alikiuka kiapo cha uaminifu wa kazi hatua ambayo ilihujumu imani ya wananchi na hakutaja mwenendo wake kuwa ndoto ya ajabu kwa waanzilishi wa taifa.**

Bunge hilo linaloongozwa na chama cha upinzani cha Democrats, lilipiga kura ya kutokuwa na imani na rais mwezi uliopita.

Bunge la Seneti linaloongozwa na Chama cha Republican cha Rais Trump litaamua ikiwa atashtakiwa na kuondolewa madarakani.

Katika stakabadhi zenye kurasa sita jopo la mawakili wa Rais Trump liliwasilisha hoja wanazotarajia kutumia kama katika kesi hiyo.

Jopo hilo la wanasheria, linaloongozwa na wakili wa Ikulu ya Marekani, Pat Cipollone na Wakili wa kujitegemea wa Rais Trump, Jay Sekulow, lilisema kuwa linapinga kesi ya kutaka kumwondoa Rais Trump madarakani kwa misingi ya kutofuata kanuni na ukiukaji wa katiba, likidai kuwa Rais Trump hakufanya kosa lolote na kwamba anaonewa.

Katika maelezo yaliyowasilishwa Jumamosi, Democrats walielezea kwa kina kwanini wanataka Rais Trump aondolewe ofisini.

Walisema kuwa Rais Trump alikiuka kiapo cha uaminifu wa kazi hatua ambayo ilihujumu imani ya wananchi na hakutaja mwenendo wake kuwa ndoto ya ajabu kwa waanzilishi wa taifa.

Katika mawasiliano ya simu, Rais Trump alimtaka Zelensky amchunguze Joe Biden, ambaye kwa sasa ndiye mgombea aliye mstari wa mbele kuwania kiti cha urais kwa tiketi ya chama cha Democratic katika uchaguzi wa urais mwaka ujao, na mtoto wake wa kiume, Hunter Biden, ambaye awali alifanya kazi kampuni ya nishati ya Ukraine Burisma.

Uchunguzi unataka kubaini ikiwa Rais Trump alitumia kitisho kuzuia msaada wa Jeshi la Marekani kwa Ukraine ili kuifanya imchunguze Biden na mwanawe.

Hata hivyo, Rais Trump amekana kufanya kosa lolote na ameutaja uchunguzi kuwa ni hila dhidi yake. **BBC**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas (kushoto), alipokutana na Jenerali Marshal Khalifa Haftar. **PICHA: REUTERS**

# Ujerumani yaandaa mkutano kutafuta amani Libya

**BERLIN,** Ujerumani

VIONGOZI kutoka mataifa mbalimbali wamekusanyika mjini Berlin jana, kujadili mpango mpya wa amani nchini Libya.

Mkutano huo wa kilele unalenga kumaliza mzozo katika nchi hiyo na kuiepusha kugeuka kuwa Syria ya pili.

Viongozi hao wamekutana mjini humo kujadili makubaliano ya kusitisha mapigano nchini Libya yanayoyumba tangu alipofariki kiongozi wa taifa hiyo, Muammar Gaddafi mwaka 2011.

Wakati huo huo washiriki kwenye mkutano huo wanataka kutafuta njia ya kukabiliana na nchi za kigeni zinazoingilia kati masuala ya nchi hiyo inayokumbwa na machafuko tangu kuzuka ghasia za kuipinga serikali za mwaka 2011 zilizoungwa mkono na nchi wanachama wa jumuiya ya kijeshi Nato.

Ujerumani na Falme za Kiarabu (UAE) zimetoa wito wa pamoja kwa pande zote katika mzozo wa Libya kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa ya kusitisha mapigano ya muda mrefu na kwa vikosi vya kigeni kuondoka nchini humo.

Msemaji wa serikali ya Ujerumani, Steffen Seibert, alisema wito huo ulitolewa baada ya kufanyika mkutano Kati ya Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel na mwanamfalme wa Abu Dhabi, Sheikh Mohammed bin Zayed al Nahyan, kabla ya mkutano wa kilele kuhusu amani ya Libya ambapo viongozi wa kimataifa wanakutana mjini Berlin mnamo Jumapili 19.

Viongozi hao wawili walisisitiza kwamba mzozo wa Libya hauwezi kutatuliwa kwa njia za kijeshi, bali kwa kudumisha amani na utulivu ambavyo vitafikiwa kwa njia ya mazungumzo.

Sheikh Mohammed bin Zayed Al Nahyan alisema Falme za Kiarabu zingefanya kila jitihada kusaidia utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa Berlin kuhusu Libya.

UAE ni mmoja wa washirika muhimu zaidi wanaomuunga mkono kiongozi wa waasi Jenerali Khalifa Haftar ambaye vikosi vyake vinadhibiti sehemu kubwa ya Libya na wanaipinga serikali ya Waziri Mkuu, Fayez al-Serraj iliyopo katika Mji Mkuu wa Libya, Tripoli inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa.

Marais wa Urusi, Uturuki na Ufaransa watafanya mazungumzo yatakayo simamiwa na Umoja wa Mataifa, ambao unataka nchi za nje zenye nguvu na ushawishi mkubwa katika eneo hilo ziache kujiingiza katika vita ya nchini Libya, kupitia utoaji wa silaha, askari au ufadhili wa fedha.

Mjumbe maalumu wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia masuala ya Libya, Ghassan Salame pia alitoa wito wa kuondolewa wapiganaji wa kigeni katika nchi iliyoghubikwa na vita kabla ya kuanza mkutano huo wa amani ya Libya unaofanyika katika mji wa Berlin. **DW**

# Takukuru yawajia juu watumishi wa afya

**Na Elisante John, SINGIDA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewaonya wataalamu wa afya vijijini, matabibu na wauguzi wanaobandika namba za simu katika milango ya ofisi zao, kwa lengo la kupigiwa na wagonjwa wanaohitaji kupewa huduma za tiba.

Imeelezwa kuwa wataalamu hao hubandika namba za simu kwenye milango ya ofisi, huku wakiendelea na majukumu yao mengine binafsi nje ya vituo vyao vya kazi, hali inayokwenda kinyume cha sheria za utumishi wa umma.

Akizungumza na watumishi wa halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Kamanda wa Takukuru wilaya hiyo, Erick Nyoni, alisema hali hiyo imekuwa ikisababishia usumbufu mkubwa kwa wagonjwa kuwatafuta madaktari.

"Nimefuatilia sana hali hii na nimebaini katika zahanati za vijiji vitatu hivi daktari ameandika kwenye mlango wa ofisi yake kuwa eti 'nipigie kwa namba hii'...sisi tukiwa watumishi wanaofuata taratibu za utawala bora, lazima kero hii tuidhibiti," alisema Nyoni.

Alifafanua kuwa daktari, muuguzi au mtumishi yeyote wa idara ya afya au serikali kwa ujumla, ni wajibu wake kuwapo karibu na eneo la kazi kwa muda wote wa saa za kazi, lakini si wajibu wa mgonjwa kuanza kumtafuta kwa simu anapokwenda zahanati, kwa ajili ya kutibiwa.

Kuhusu Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Nyoni alikemea tabia ya baadhi ya viongozi na watendaji wa vijiji na kata kuingilia majukumu ya mabaraza hayo, hali inayokwamisha haki kwa wananchi waliofungua mashauri, kwa ajili ya kutafuta haki.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, aliwataka wataalamu wakiwamo wakuu wa idara kujenga tabia ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa vijijini, badala ya kukaa ofisini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, aliahidi kuzifuatilia na kuzifanyia kazi kwa karibu zaidi kwa kushirikiana na Takukuru, ili kudhibiti matatizo yanaoikumba jamii.

Alisema ufuatiliaji huo utajumuisha kuwabaini watumishi wenye nia na kusudio la kuwaonea wananchi katika maeneo ya vijijini, hasa kupitia mabaraza ya ardhi ya kata, na hata watumishi wengine wa umma wasiopenda kutekeleza vema majukumu yao ya kazi.



Ofisa Mkusanyaji Takwimu kutoka Taasisi ya Mama Alaska Jamii, Hans Warioba, akizungumza na mama lishe wa jijini Dar es Salaam jana, wakati wa semina ya kutoa mafunzo ya mbinu za kusimamia biashara zao ili waongeze vipato. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wazazi wa watoto wasioripoti kidato cha kwanza kusakwa leo

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZAZI ambao hawajapeleka wanafunzi wa kidato cha kwanza shuleni katika Kata ya Odonyowas hadi ifikapo leo, wametangaziwa kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Elimu wa Kata hiyo, Jakobo Jackson, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ambapo alisema kuwa hadi kufikia Januari 17, idadi ya wanafunzi ambao wamechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika kata hiyo ni 160, lakini hadi sasa walioripoti shuleni ni 89 tu kitu ambacho hakiridhishi.

Alisema kuwa amewaagiza walimu kuandika majina ya wanafunzi wote ambao wamechaguliwa na hawajaenda kuripoti shuleni na hadi ikifika leo hawajaenda, wataanza msako wa nyumba kwa nyumba kuangalia kwanini wanafunzi hao hawajaripoti shuleni hadi sasa na iwapo ikijulikana ni uzembe wa mzazi hatua kali itachukuliwa dhidi yake.

"Kwa kweli hatutanii, haiwezekana Rais wetu aweke kipaumbele kwa watoto wetu kwa kutoa elimu bure halafu unakuta mwanafunzi amefaulu vizuri, lakini haendi shule... ukiangalia sababu za msingi hamna kwa kweli nasema atutafumbia macho mzazi ambaye ajampeleka shule mototo wake," alisema na kuongeza:

"Tutapita nyumba kwa nyumba na ikibainika basi lazima sheria ifuate mkondo wake dhidi ya mzazi wa mwanafunzi aliyefaulu na hajampekeleka shuleni."

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Odonyowas, Richard Mugyabuso, alisema kuwa hadi sasa shuleni kwake amepokea wanafunzi 89 na walitakia kuripoti wanafunzi 169 wa kidato cha kwanza, na kuwa hiyo inaonyesha jinsi mwamko wa wanafunzi kwenda shuleni ni mdogo sana kwani zaidi ya wanafunzi 80 hawajafika shuleni hapo na hakuna taarifa yoyote aliyoipata kutoka kwa wazazi.

"Tumepewa maelekezo hadi ikifika Jumatatu (leo) tupeleke majina yote ya watoto ambao hawajafika shuleni katika ofisi ya kata, ili msako wa wazazi ambao hawajawaleta watoto shuleni uanze, na sababu ya kutokuja ijulikane... hii itawasaidia wanafunzi wote kuja shuleni," aliongeza.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wamekwenda na kuripoti shuleni ili kuondokana na matatizo ambayo yanaweza kuwapata ikiwamo kuchukuliwa hatua za kisheria.

## Wahitimu watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Romana Mallya**

WAHITIMU wa vyuo vikuu, taasisi na kampuni mbalimbali wametakiwa kuchangamkia fursa zilizopo kwenye nishati jadilifu, ili kukabiliana na changamoto ya ajira na kuongeza nguvu ya uchumi wa viwanda.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng'i Issa, wakati akizindua huduma ya kiatanishi cha biashara zinazohusika na nishati jadilifu awamu ya pili.

Huduma hiyo ambayo imeandaliwa na Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED) itatekelezwa kwa muda wa miaka miwili na washiriki watano watakofanya vizuri watapelekwa nchini India kuongeza ujuzi.

Alisema huduma hiyo ni mwendelezo wa ile ambayo imekuwa ikitolewa kuanzia mwaka 2014, kwa ushirikiano na Norges Vel na ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Norad Norway (NORAD).

"Nimeambiwa huduma ya sasa inatolewa kwa ushirikiano na mifuko ya Selco Foundation wa nchini India na ufadhili wa CS Mott Foundation," alisema na kuongeza:

"Wahitimu vyuoni ninawashauri watumie fursa hii kujiunga na kiatanishi hiki kwa kuanzisha huduma mbalimbali za umeme wa jua... hii ni sekta inayokua na kama mnavyofahamu tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda."

"Hakuna viwanda bila nishati na hatuwezi kuendesha viwanda kwa kutegemea nishati ya aina moja ni muhimu kuziendeleza nishati hizi."

Kwa mujibu wa Issa, fursa hiyo ni muhimu kwa sababu ili mtu apige hatua anahitaji kuongeza ujuzi hasa kutoka kwa nchi nyingine.

Alizitaka taasisi, kampuni na wadau wengine wa nishati hiyo wawe na utayari wa kushiriki huduma hiyo itakayoendeshwa kwa kipindi hicho cha miaka miwili.

"Upo mfuko unaotoa mikopo kwa riba nafuu ambao unafanya kazi kwa ushirikiano na Benki ya NBC na CRDB ambao wanufaika wake ni wale wanaozalisha kutumia nishati ya jua, nimeongea haya kwa sababu unawahusu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa IMED, Dk. Donath Olomi, alisema mpaka sasa katika awamu ya kwanza walioomba ni 32. Alisema baada ya kupokea maombi watayapitia na kuyachuja na kubakiwa na watu 14 ikiwa ni awamu ya kwanza na lengo ni kukuza biashara za nishati jadilifu ili kufikia watu wengi zaidi.

"Tutatoa huduma za kuandaa mipango ya kukuza biashara, ushauri, mafunzo ya ufundi na ya biashara na kuunganisha masoko," alisema.

Dk. Olomi alisema kwa walioko mkoani watapata huduma kutoka Dar es Salaam na kupitia mtandao wa wawezeshaji wa IMED waliopo katika mikoa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAKAME ALLY MAKAME** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA HAICE trim yenye namba za usajili T 320 CQU. rangi nyeupe.

Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/104665/2019.

### PASSPORT IMEPOTEA



115590402

**HILDA RICHARD TESHA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB 328383.** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2009. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **KAWE/RB/362/2020.**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S. M. M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo Dodoma Mjini**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NA 6/2020**

**Ombi la Snifa Shaban kuteuliwa**

Msimamizi wa mirathi marehemu Musa Ramadhan Rajabu

Kwa yeyote Anayehusika
Tanzania Bara

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuhudhuria kesi wakita mnamo tarehe 3/2/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa 13/1/2020


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako*

*la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ARTETA ALIA KUGAWA POINTI

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Arsenal "imetoa pointi mbili ugenini" baada ya bao la dakika za mwisho la John Fleck kuiwezesha Sheffield United kupata sare ya 1-1 kwenye Uwanja wa Emirates na aliilaumu safu ya ulinzi.

Gabriel Martinelli aliwaweka mbele 'Washika Bunduki' hao wakati akifunga bao lake la tisa msimu huu mwishoni mwa kipindi cha kwanza Jumamosi na Arsenal iliendelea kutawala mpira hadi dakika 10 za mwisho.

Arteta alishuhudia krosi ya Callum Robinson ikimkuta Fleck, ambaye alifunga na kusawazisha.

"Nimekatishwa tamaa. Tumetoa pointi mbili," alisema bosi huyo wa Arsenal.

"Kuna historia ya kutoa mabao ugenini. Kwenye Ligi Kuu wakati ukiwa unaongoza kwa 1-0 chochote kinaweza kutokea.

"Nafikiri wote walicheza vizuri. Pengine kipindi cha kwanza tulitakiwa kuwa na mabao mengi zaidi ili kumaliza mchezo ambao tuliutawala kila sehemu."

Huku Kieran Tierney na Calum Chambers wakiwa majeruhi, Arteta alimchagua Ainsley Maitland-Niles na Bukayo Saka na akabainisha kwamba makosa yake yalichangia kupata sare hiyo.

"Wakati tukiwajadili wapinzani wetu tunaweza kuwauliza Ainsley na Bukayo vitu vingi, lakini wao si mabeki wa pembeni," alisema Arteta.

# Madrid wamfungia kazi Mbappe

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kwamba, inajiandaa kutoa dau la pauni milioni 257 ili kunasa saini ya nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto.

Inaelezwa baada ya kukaa PSG kwa miaka mitatu, Mbappe sasa yuko tayari kujiunga na Real Madrid ili kupata changamoto mpya katika ligi yenye ushindani mkubwa zaidi ya ile ya Ufaransa.

Licha ya Mbappe kubakiza miaka miwili na nusu kwenye mkataba wake wa sasa PSG, Real Madrid inajiandaa kuvunja rekodi ya usajili ili kunasa saini ya straika huyo.

Madrid imepanga kuweka mezani pauni milioni 257 ili kumnasa Mbappe, dau ambalo litavunja rekodi ya sasa ya usajili ya pauni milioni 198 ambayo PSG ilitumia kumsajili Neymar kutoka Barcelona.

Mbappe amekuwa na wakati mzuri kwenye kikosi cha PSG na klabu nyingi kubwa barani Ulaya zimekuwa zikihusishwa na kuitaka huduma yake ikiwamo Liverpool. Hata hivyo, kinachosubiriwa ni kwa klabu yenye nguvu na Madrid inaonekana itaishinda vita hiyo.





# *Mourinho ajiuliza kusajili mshambuliaji*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema hana hofu ya kumsajili mshambuliaji kwa gharama yoyote wakati akitaka kubakia kuwa na "imani" kwa wachezaji wake sasa wa Tottenham.

Mshambuliaji wa Milan, Krzysztof Piatek, nyota wa Porto, Ze Luis na mshambuliaji wa zamani wa Spurs, Fernando Llorente wamekuwa wakihusishwa na kusajiliwa kipindi hiki cha Januari, baada ya kuumia kwa Harry Kane.

Tottenham walitoka sare ya bila kufungana na Watford Jumamosi na Mourinho anahisika walitakiwa kushinda mchezo huo kama wangekuwa na Kane au mshambuliaji yeyote dimbani.

Lakini kocha huyo alibainisha kwamba hawezi kupaniki kwenye soko la usajili, kwani anahitaji utulivu kwanza.

"Kama inawezakana sawa, kama haiwezekani sawa," alisema Mourinho akizungumza kuhusu usajili wa mshambuliaji wakati huu wa dirisha dogo la usajili, ambapo Spurs imecheza mechi nne mfululizo bila ushindi kwenye Ligi Kuu.

"Wote tunajua, wote tunataka mambo mazuri kwa timu, vitu bora kwa klabu. Ndivyo inavyotakiwa.

"Laini tunatakiwa kufanya vitu ambavyo vinawezekana na ambavyo vipo sawa kuvifanya. Hii si mechi ya mwisho kwenye historia ya Tottenham. Jumatano tuna mchezo mmoja, na msimu ujao tunayo mingi tu.

# HABARI MICHEZO

## Gattuso: Napoli kujifua zaidi baada ya kipigo

**NAPLES,** Italia

GENNARO Gattuso amesema wachezaji wa Napoli wameamua kwenda kujifua zaidi kwenye mazoezi baada ya kufungwa mabao 2-0 nyumbani na Fiorentina.

Napoli ilikumbana na kipigo hicho Jumamosi dhidi ya Fiorentina – na kilikuwa kipigo cha tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kuiacha timu hiyo inayonolewa na Gattuso ikiwa nafasi ya 13.

Gattuso amepoteza mechi nne kati ya tano tangu aanze kuinoa timu hiyo baada ya kuchukua mikoba ya Carlo Ancelotti Desemba mwaka jana.

Sasa Napoli wanakwenda kwenye mazoezi ya kujifua zaidi kuelekea mchezo dhidi ya Lazio na Juventus, alibainisha kocha Gattuso baada ya mchezo huo.

Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis alichukua hatua wakati nyota wa kikosi cha kwanza kuripotiwa kugomea mazoezi wakiwa chini ya Ancelotti mapema mwanzo mwa msimu huu.

"Nimezungumza na kikosi na wameamua kufanya maamuzi ya kwenda kwenye mazoezi ya kujifua zaidi jioni," alisema Gattuso akiiambia Sky Sport Italia.

"Yalikuwa maamuzi yao. Hatuwezi kuidharau timu yoyote. Tunatakiwa kuangaliana kila mmoja machoni, kukaa pamoja na kusema kile kinachopaswa kusemwa."





## ZIDANE: APONGEZA VAR KUKATAA BAO LA DE JONG

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anaamini yalikuwa maamuzi sahihi kulikataa goli la Luuk de Jong wakati Real Madrid ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Sevilla, Jumamosi.

Madrid walipaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wakati mabao mawili ya Casemiro yalipowahakikishia pointi tatu katika mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Santiago Bernabeu, licha ya De Jong kufunga na kufanya matokeo kuwa 1-1 kipindi cha pili.

Mshambuliaji huyo alifikiri kwamba aliipa Sevilla uongozi, lakini mpira wake wa kichwa haukuruhusiwa na VAR, huku mwamuzi Juan Martinez Munuera akimpa adhabu ya penalti Nemanja Gudelj kwa kumzuia Eder Militao.

Kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui alionyesha kutoridhishwa na maamuzi hayo na mkurugenzi wa soka, Monchi alidai angeitoa timu uwanjani kama angeona bao jingine lisingeruhusiwa na VAR wakati lile la Munir El Haddadi ambaye awali alionekana kama kaunawa mpira, kuruhusiwa.

Lakini Zidane anaona kwamba ilikuwa ni sawa kabisa kukataliwa kwa bao hilo kama VAR ilivyoonyesha.

## *Haaland aanza na 'hat-trick' Dortmund*

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland ameanza vizuri zaidi katika mchezo wake wa kwanza kuichezea Borussia Dortmund kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, baada ya kufunga 'hat-trick' ya haraka.

Haaland aliingia akitokea benchi kipindi cha pili na akafunga mabao matatu ndani ya dakika 20 wakati Dortmund wakiisambaratisha Augsburg kwa mabao 5-3, juzi Jumamosi.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye alisajiliwa kwa euro milioni 20 kutoka Salzburg Januari mwaka huu akichukua nafasi ya Lukasz Piszczek katika dakika ya 56 na alifunga baada ya kuugusa mpira kwa mara ya kwanza baada ya sekunde 183 kabla ya kuongeza mengine mawili.

"Ilikuwa siku nzuri, nina furaha kubwa. Kwa sasa nimetulia sana, sijui kwa nini," alisema Haaland, ambaye pia alikuwa akihushwa na mpango wa kutua kule Manchester United na RB Leipzig kabla ya kujiunga na Dortmund, akiambia Sky.

"Mbinu zilikuwa nzuri. Nina watu wazuri wanaonizunguka mimi hapa Dortmund, nina wachezaji wenzangu wazuri na ni klabu inayovutia mno. Naweza kucheza leo, hilo ndio jambo muhimu zaidi."

Haaland amekuwa mchezaji wa kwanza wa Dortmund kufunga hat-trick kwenye mchezo wake wa kwanza tangu Pierre-Emerick Aubameyang mwaka 2013. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alifunga mabao 28 katika mechi 22 alizocheza kwenye mashindano yote katika Klabu ya Salzburg katika nusu ya kwanza ya msimu wa 2019-20.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ZAHA ASIRUHUSIWE KUKIMBIA - GUARDIOLA

## Hutakiwa kumruhusu, si rahisi na tuliruhusu hilo, tulishindwa kutulia...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola ameilaumu safu yake ya ulinzi kwa kucheza vibaya na kuwaruhusu Crystal Palace kupata sare ya 2-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England katika dimba la Etihad, Jumamosi.

**Wenyeji hao walikuwa nyuma baada ya Cenk Tosun kufunga bao la ufunguzi dakika ya 39, lakini Sergio Aguero alisawazisha na kufunga la pili huku akifikisha mabao 250 akiwa katika jezi ya City, zikiwa zimesalia dakika nane mpira kumalizika.**

Kujichanganya kwa beki John Stones kushindwa kumzuia Wilfried Zaha kukafanya beki Fernandinho ajikute akisukumiza mpira wavuni mwao na kuwapa sare hiyo Palace.

"Tunatakiwa kuepuka makosa tuliyoyafanya katika bao lao la pili," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Hutakiwa kumruhusu Zaha kukimbia, si rahisi. Na tuliruhusu hilo.

"Hapana, haikuwa kwamba tulishindwa kutulia, yalikuwa ni maamuzi. Utulivu ulikuwa pale. Tutalimaliza hili na tutaimarika vizuri tu.

"Katika nafasi zile tulihitaji kuwa na mabeki wanne nyuma na kutowaruhusu wao kufanya mashambulizi ya kushtukiza." Ingawa hakumtaja beki wa kimataifa wa England, Stones wa kutokuwa makini, lakini ilionyesha dhahiri kwamba, lawama za Guardiola zilikuwa dhidi ya beki huyo ambaye bado hayupo fiti.

Mwishoni mwa mchezo huo, Stones alionekana kama aliyeumia goti, lakini Guardiola hakutoa taarifa yoyote kuhusu hilo.

"Sijaonana na madaktari. Sasa tunakwenda kuangalia," alisema.

City ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, sasa wamepitwa pointi 13 na vinara Liverpool ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Manchester United.

Hata hivyo, Guardiola hakutaka kuzungumzia kama mbio za ubingwa wa ligi hiyo bado upo kwa timu yake na badala yake akasisitiza anaungalia zaidi mchezo unaofuata wa kesho, Jumanne dhidi ya Sheffield United.

"Nimelijibu swali hili zaidi ya mara milioni kwa wiki kadhaa zilizopita," aliongeza.

## ZISIKUPITE

### CAN AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton inaandaa ofa ya pauni milioni 30 kwa ajili ya kumnasa Mjerumani Emre Can, 26, ambaye ni kiungo wa zamani wa Liverpool, kwa sasa hana nafasi pale Juventus. ***(Sunday Mirror)***

### LIVER, CHELSEA KWA WERNER

LIVERPOOL itatoa changamoto kwa Chelsea kumwania nyota wa RB Leipzig mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner. ***(Sunday Mirror)***

### MKURUGENZI LILLE KUULA UTD

MKURUGENZI wa soka wa Klabu ya Lille, Luis Campos anapewa nafasi kubwa ya kwenda kuchukua nafasi kama hiyo pale katika Klabu ya Manchester United. ***(Sun on Sunday)***

### ARSENAL KUMKOSA KURZAWA

KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel amesema klabu yake inahitaji kumbakiza beki wa kushoto Layvin Kurzawa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akiwaniwa na Arsenal. ***(Goal)***

### MADRID YAIPIKU MAN UTD

KLABU ya Manchester United imezidiwa ujanja na Real Madrid kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Ajax na Uholanzi, Donny van de Beek, mwenye umri wa miaka 22. ***(Daily Star Sunday)***

### ARSENAL MGUU KWA BRUNO

MKURUGENZI wa Ufundi wa Arsenal, Edu amekutana na wawakilishi wa Athletico Paranaense kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kumsajili kiungo mkabaji, Bruno Guimaraes anayetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 25.6 ambaye ana umri wa miaka 22 na raia wa Brazil. ***(Goal - in Portuguese)***

### PSG YAJITOSA KWA KOULIBALY

KLABU ya PSG ipo tayari kutoa ofa ya kumsajili beki wa kati wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake utakuwa na thamani ya pauni milioni 10.2 kwa mwaka kama ataondoka Napoli. ***(Foot Mercato - in French)***

### MOURINHO KUSAJILI STRAIKA

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho ana matumaini ya kusajili mshambuliaji kipindi hiki cha dirisha la Januari, huku mshambuliaji wa kimataifa wa England, Harry Kane akiwa nje kutokana na kuwa majeruhi. ***(Evening Standard)***

### CAVANI KULAZIMISHA KUSEPA

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 32, atawaomba Paris St-Germain kuharakisha uhamisho wake wa kwenda Atletico Madrid. ***(Marca)***

### ROMA HESABU KWA JANUZAJ

KLABU ya Roma inataka kumsajili winga wa zamani wa Manchester United, Adnan Januzaj kwa mkopo kutoka Real Sociedad, huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja raia huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 24, katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail on Sunday)***

HABARI MICHEZO

# Katwila atazama alipoangukia KMC

Na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila (pichani) amesema licha ya kupoteza mchezo uliopita, bado anaimani ya kushika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi kwa kuichapa Simba bao 1-0 kwenye mechi ya fainali, Mtibwa ilikuwa ikipewa nafasi nzuri ya kuendeleza ushindi kwenye Ligi Kuu Bara, lakini ikajikuta ikiangukia pua kwa kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya KMC FC.

Akizungumza na Nipashe Jana, Katwila alisema vijana wake walionyesha upungufu mkubwa katika mchezo huo wa ligi uliopita, lakini ataendelea kuisuka na kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili kufanya vizuri.



Katwila alisema vijana wake hawakucheza vizuri kama ambavyo alivyotegemea lakini akaahidi kuyafanyia kazi kasoro alizozibaini.

"Naendelea kukifanyia marekebisho kikosi changu ili kifanye vizuri na kuendelea kubakia kwenye msimamo wa Ligi Kuu," alisema Katwila na kuwataka mashabiki wao kuendelea kutoa ushirikiano katika timu hiyo.

"Tunaomba mashabiki waendelee kutusapoti ili tutimize ndoto yetu ya kubakia Ligi Kuu."



Balozi wa Sayona Twist, Rajabu Abdul Kahali maarufu Harmonize, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya uzinduzi wa kinywaji cha Sayona Twist uliofanyika wiki iliyopita jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Motisun Group, Subhash Patel, Mkurugenzi Mtendaji wa Motisun Group Veer Patel, Mkurugenzi Mtendaji wa Sayona Drinks Limited, Pawan Patel, Mkurugenzi Mkuu wa Sayona Group, Nitin Menon na Meneja wa Harmonize, Sebastian Ndege maarufu Jembe ni Jembe. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NYOTA YANGA AOMBA 'SUBRA' KWA MASHABIKI

Na Shufaa Lyimo

BEKI wa Yanga, Juma Abdul amewataka wanachama wa klabu hiyo kutulia na kutokatishwa tamaa na matokeo wanayoyapata uwanjani kwa kuwa ndiyo kwanza timu hiyo inajengwa.

**Juzi Yanga ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Azam FC kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa, matokeo hayo yakija baada ya mchezo uliopita kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya timu hiyo kukubali kipigo cha pili mfululizo wakiwa chini ya Mbelgiji Luc Eymael, alisema kwa sasa bado hawajauzoea mfumo wa kocha huyo mpya ambaye hiyo ni mechi yake ya pili tangu atue.

"Ninaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano, wasikatishwe tamaa na matokeo yaliyopita, kidogo kidogo tutamzoea kocha wetu," alisema Abdul.

Akizungumzia mchezo huo dhidi ya Azam FC ambao waliibuka na ushindi baada ya beki Ally Mtoni Sonso kujifunga, alisema walifanya makosa yaliyosababisha kukosa pointi tatu muhimu.

Alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, ambapo wapinzani wao walitoa presha kubwa langoni mwao na kubahatika kupata bao hilo.

"Wenzetu walitumia nafasi zao vizuri wakatoka na pointi tatu mpira ndivyo ulivyo, kikubwa tunajipanga kwa ajili ya mchezo ujao," alisema.

Alisema kwa sasa wanajipanga kukutana na timu ya Singida United kesho kutwa katika mchezo utakaopigwa mkoani Singida.

Alisema amejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo akiwa na lengo la kuipa ushindi timu yake.

Matokeo hayo yameifanya Yanga kukaa katika nafasi ya saba ikiwa na alama zake 25 baada ya mechi 14, wakati Azam iliyoshuka dimbani mara 15 na kukusanya alama 32, ikikaa katika nafasi ya pili nyuma ya vinara Simba wenye pointi 41 zilizotokana na mechi 16 msimu huu.

Meneja wa Ufundi Mauzo ya Jumla wa Zantel, Efrem Akwilini (kulia), akikabidhi zawadi ya simu aina ya SMARTA kwa Isack Daud, mshindi wa jumla wa mashindano ya wiki ya gofu yaliyoandaliwa na kampuni ya mawasiliano ya Zantel na kufanyika katika viwanja vya TPDF Lugalo Golf Club jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, (katikati mwenye fulana nyekundu) ni Mwenyekiti wa Chama cha Gofu nchini, Chriss Martin na Brigedia Jenerali Kondwani Kalino. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



# Tanzania Wanawake U-20 waifumua Uganda

Na Mwandishi Wetu

Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20 imeibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya timu ya Taifa ya Uganda kwenye mchezo uliochezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana.

Katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Costa Rica na Panama kuanzia Julai 2-22, mwaka huu, hadi kipindi cha kwanza kinamalizika hakuna timu iliyoweza kuona lango la mwenzake.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi kwa timu zote kutafuta bao la kuongoza na mipango ya Uganda ilianza kufanikiwa kufuatia kuanza kutupia kupitia kwa Nalukenge Juliet dakika ya 47. Bao hilo liliwaamsha wachezaji wa Tanzania na katika dakika ya 58, wakasawazisha kupitia kwa Diana Lucas akimalizia pasi ya Asha Masaka.

Uzembe wa mabeki wa Uganda dakika ya 68 uliwapa zawadi ya kona Tanzania iliyopigwa na Diana Lucas na ikazamishwa kimiani na Opah Clement.

Tanzania sasa itahitaji sare ama ushindi wowote katika mechi ya marudio inayotarajiwa kuchezwa Februari Mosi, mwaka huu nchini Uganda ili kusonga mbele.

Michezo
Jumatatu Januari 20, 2020
Nipashe



Zaha asiruhusiwe kukimbia - Guardiola

HABARI UK.30

RAHA SANA...



Wachezaji wa timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 20, wakishangilia baada ya kupata bao la ushindi dhidi ya Uganda wakati wakishinda 2-1 kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Julai mwaka huu, iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. P**ICHA: JUMANNE JUMA**

# Sonso aiangukia Yanga, TFF, Azam FC

**Na Mwandishi Wetu**

BEKI wa Yanga, Ally Mtoni Sonso, ameiangukia familia ya soka baada ya kufanya makosa ya 'kitoto' katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC juzi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo ambayo, Azam ilishinda kwa bao 1-0 lililotokana na Sonso kujifunga, beki huyo aliigharimu timu yake baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu dakika ya 80 hivyo kulazimika kucheza pungufu.

Sonzo alimchezea rafu beki wa Azam FC, Mganda Nicolaus Wadada na wakati akiwa chini akaonekana akimkanyaga kama vile amedhamiria.

Kupitia mtandao wa kijamii, Sonso aliandika: " Naomba msamaha wanamichezo wote kwa kadi niliyoipata kwa siku ya jana [juzi] na tukio nililolifanya kwenye mchezo wetu dhidi ya Azam FC.

"Ni kweli mchezo wa mpira ni mchezo wa furaha na upendo kwa kuwa ni ajira, ila changamoto za hapa na pale zipo, pia naomba msamaha kwa wachezaji, viongozi wangu wa @ yanga na pia hata wa @azamfcofficial na hata viongozi wenye dhamana na soka letu @tanfootball na sitaweza kurudia tukio la aina ile."

# Simba yasambaratisha tena

## Mkude, Dilunga upepo wa Kirumba wawanyookea, Kagere akimbiza kileleni huku Chama...

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Simba imeongeza pengo la pointi kwa wapinzani wake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kuisasambua Alliance FC ya Mwanza kwa mabao 4-1 kwenye mechi kali iliyochezwa jana Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

**Simba imefikisha pointi 41 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa imeizidi Azam FC inayokamata nafasi ya pili kwa pointi tisa, kwani baada ya kuifunga Yanga Jumamosi iliyopita imefikisha jumla ya alama 32.**

Simba imeshacheza mechi 16, ikibakisha mechi mbili tu kumaliza mzunguko wa kwanza, huku Azam ikiwa imecheza mechi 15, ikibakisha mechi tatu kuhitimisha mzunguko huo. Haikuwa kazi rahisi kwa Simba kwani ilitanguliwa kufungwa bao, lakini ilipambana kufa kupona kuhakikisha inapata pointi tatu na kufurahisha mashabiki wake waliojazana uwanjani hapo kuishangilia.

Licha ya Simba kufanya mashambulizi mengi langoni mwa Alliance FC, lakini tatizo kubwa lilikuwa ni umakini na papara kwa wachezaji wake walipokuwa wakifika eneo la hatari, huku wakitatizwa na mfumo wa wapinzani wao waliokuwa wamepaki basi na kushambulia kwa kushtukiza.

Baada ya kushambulia sana na kukosa mabao, waliadhibiwa kwa bao hilo la dakika ya 27, lililofungwa na Israel Patrick kwa mkwaju wa faulo.

Ilitokana na shambulio la kushtukiza na Erasto Nyoni kucheza madhambi nje kidogo ya eneo la hatari, lakini wakati faulo hiyo ikipigwa akafanya makosa ya kuhama eneo alilokuwa na mpigaji kupenyeza mpira uliozama kimyani.

Wakati kila mmoja akijua Alliance FC itamaliza dakika 45 za kwanza ikiongoza, kiungo Jonas Mkude aliisawazishia Simba bao, baada ya kutoka heka heka langoni na mpira ukamkuta mfungaji aliyepiga mpira wa pembeni kwa ufundi, ukajaa wavuni, ikiwa ni dakika ya mwisho, kabla ya kukamilika dakika tatu za nyongeza.

Bao hilo ni la pili kwa Mkude katika Uwanja wa CCM Kirumba msimu huu baada ya mechi iliyopita dhidi ya Mbao FC kufunga pia wakati wakishinda 2-1.

Meddie Kagere ambaye kwa mechi kadhaa sasa hajafunga bao lolote, aliiandikia timu yake bao la pili kwa kichwa dakika ya 58, baada ya kumalizia kichwa kilichopigwa na beki Paschal Wawa, kufuatia faulo iliyopigwa na Claotus Chama, hilo likiwa ni bao lake la 11 kwenye ligi hiyo msimu huu.

Dakika tatu baadaye, Chama aliiandikia Simba bao la tatu kwa mkwaju wa faulo, baada ya yeye mwenyewe kufanyiwa madhambi karibu na eneo la hatari, kabla ya kupiga mpira uliokwenda moja kwa moja hadi wavuni.

Hassan Dilunga kama ilivyo kwa Mkude, naye alifunga bao lake la pili msimu huu katika Uwanja wa CCM Kirumba baada ya kuwa mfungaji kwenye mechi dhidi ya Mbao. Dilunga alipigilia msumari wa mwisho dhidi ya Alliance, alipofunga bao la nne dakika ya 72.

Mfungaji alitanguliziwa mpira mrefu ambao kipa wa Alliance, John Mwenda alitoka kutaka kuuwahi, lakini Dilunga akibetua kwa juu na kudondokea wavuni.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >